# MSAMAHA

Na tuendelee kusimama kwa muda kidogo tu kwa ajili ya maombi. Na tuinamishe vichwa vyetu sasa.

2 Baba yetu wa Mbinguni, tunayahesabu haya kuwa majaliwa makubwa mno kusimama hapa miongoni mwa waliookoka, na tunaweza kuimba wimbo huu mtukufu wa kale wa Kanisa, "Bwana, ninaamini." Kuona Imani ya baba zetu ingali ikiishi mioyoni mwa watoto Wake, kote katika nyakati. Na kama vile huo wimbo ndio kwanza utuambie, "Tuko njiani mwetu kwenda Nchi ya Kanaani." Tunaomba, Baba, usiku wa leo, kama kuna wengine hapa ambao hawajafanya uamuzi huo bado, ambao hawajafikia mahali ambapo—ambapo wanaweza tu kuliamini Neno, ninaomba ya kwamba huu utakuwa ndio usiku ambao watatoa msemo huo wa mwisho na kumkubali Kristo kama Mwokozi, wajazwe na Roho Wake.

3 Tunakushukuru kwa ajili ya kundi hili linaloitwa Wafanyabiashara wa Full Gospel, na kwa yale linayotetea, kwa ajili ya haki. Tuna furaha kujua ya kwamba nchini mwetu mna watu, katika ulimwengu wa biashara, ambao huchukua wakati kukutumikia Wewe, kuwaambia wengine, wakitumia pesa za—zao na wakati wao kuwasaidia wengine safarini, wakifanyika wenyeji wa Ufalme wa Mungu.

4 Tunakushukuru kwa ajili ya ndugu zetu wahudumu hapa usiku wa leo, hao wanaoushikilia mwenge wa nuru, kuuonyesha ulimwengu huu wenye giza kuna barabara inayoelekeza Utukufuni, kwa ajili ya kila mshirika wa Kanisa la Mungu aliye hai, na kwa wale ambao wameingia, Bwana, waliokuja kwa mara ya kwanza. Tunaomba sasa kwamba tunapojitahidi kulifungua Neno, ya kwamba utaligawa Hilo kwa watu jinsi tulivyo na haja. Ndipo wakati ibada ikiisha, usiku wa leo, nasi twende nyumbani, jalia kuweko na watoto waliozaliwa upya watakaoongezewa kwenye Ufalme. Ama, labda yupo mtu fulani hapa usiku wa leo, Bwana, ambaye ni mgonjwa sana na anahitaji mguso wa yule Tabibu Mkuu, jalia waupokee usiku wa leo. Tujalie, Bwana. Nasi kwa unyenyekevu tutakupa Wewe sifa, kwa kuwa tunaomba hayo katika Jina la Yesu, Mwana Wako. Amina.

Mwaweza kuketi.

5 Ni mmoja wa nyakati kuu sana ya maisha yangu, ni wakati nipatapo kusimama mbele za watu, kuzungumza juu ya furaha ya maisha yangu, Yesu Kristo, yale Yeye anayomaanisha kwangu, na halafu kuwa na majaliwa ya kushiriki furaha hii pamoja na mtu mwingine ambaye kamwe hajawahi kupata furaha hii. Nilikuwa nikizungumza hivi majuzi. Nilikuwa ni

mhubiri mvulana. Hii ni miaka thelathini na mitatu hudumani. Na niliishi juu ya sifa ya mhubiri mvulana. Bali sasa nimepita wakati huo, na sasa ninakuwa mhubiri mzee.

6 Bali, kila siku, Yeye, kama wimbo ulivyosema, "Yeye angali anazidi kuwa mtamu kuliko alivyokuwa siku iliyotangulia." Nilipoanza, nikavuka alama ya nusu na kutazamia machweo ya jua, Kristo anakuwa zaidi kwangu, siku baada ya siku. Basi nikiwa na majaliwa haya, kusimama mbele za wafanyabiashara wanaume na wanawake wa jamii, na kuwazungumzia kuhusu kitu ambacho kinamaanisha mengi kwao kuliko—kuliko chochote ulimwenguni, hicho ni, Uzima wa Milele. Sidhani kuna chochote kikubwa zaidi, kuliko hicho ambacho ningeweza kuwazia, kuliko Uzima wa Milele.

7 Wakati ukiwa kijana, unaanza kuwaza kuhusu, vema, kama mvulana unacheza pia, na msichana mdogo anakata wanasesere wa karatasi. Baada ya kitambo, ni elimu yako. Halafu, je! unaenda kumwoa msichana mwenye macho ya hudhurungi au samawati? Na halafu nyumba inahitaji kulipiwa, watoto wanapaswa kuelimishwa. Basi uko wapi?

8 Bali nina furaha sana kwamba kuna kitu kilicho halisi, baada ya haya yote kuisha. Ndipo unaingia ndani ya kitu fulani kinachomaanisha zaidi ya vitu hivi vingine. Ambacho, hivyo ni—hivyo vinahitajika. Hakika vinahitajika, kwake yule anayeenda kuwa mama wa nanii wetu. . .na baba wa watoto wetu, na nyumba zetu na kadhalika, na elimu ya watoto. Lakini, hata hivyo, vyote huangamia. Vinatoweka. Bali Uzima wa Milele ndio kitu kikubwa kuliko vyote nijuacho. Uliniridhisha nilipokuwa mvulana mdogo. Huniridhisha sasa nikiwa na umri wa makamu. Nami nina hakika wakati mapazia yanaposhuka kuzunguka maisha yangu, nitakuwa na furaha kwenda kukutana na Yule ambaye nimetumia maisha yangu kwa ajili yake.

9 Sasa, kwa Ndugu Tony, ra—rais wa tawi hili hapa, na nina furaha kuwa hapa pamoja na yeye katika ushirika usiku wa leo, pamoja na Ndugu Carl Williams na wenye vyeo wengine wa tawi au wawakilishi, na pamoja na nyinyi nyote wageni pamoja nasi. Tuna furaha kuwa hapa.

10 Wakati mmoja nilikuwa nikizungumza, ninaamini ilikuwa kwenye Little Rock, Arkansas, katika Ukumbi wa Kumbukumbu ya Robinson. Na kulikuwa na mtu aliyeponywa, alishakuwa kwenye mikongojo miaka kadhaa, ameketi mtaani, akiuza penseli. Na angeweza, loo, kusokoteka tu. Viungo vyake vilikuwa vimepooza. Na kuja huku. . .Watu walimhurumia sana. Usiku mmoja alikuja mkutanoni. Ndipo akapata kadi ya maombi, na kuingia mstarini na akaponywa.

11 Basi siku iliyofuata alikuwa amebeba mikongojo yake mgongoni mwake, akitembea huku na huku mtaani, akishuhudia. Nami nilikuwa nikijaribu kuzungumza. Ndipo—

ndipo baada ya kitambo akaamka, naye akasema, “Ndugu Branham,” akasema, “Kwa namna fulani niko kwenye mwisho wa akili.” Akasema, “Nilipokusikia ukizungumza,” akasema, “nilifikiri ulikuwa ni Mnazarayo.” Hicho ndicho alichokuwa. Tena akasema, “Ndipo basi nikaona Wapentekoste wengi sana pande zote,” akasema, “mtu fulani alisema ulikuwa ni Mpentekoste. Na ndipo nikakusikia ukisema kwamba ulikuwa Mbaptisti, ama uliwekwa wakfu katika kanisa la Kibaptisti.” Kasema, “Ninachanganyikiwa kabisa. Wewe ni nini?”

12 Nikasema, “Loo, hiyo ni rahisi. Mimi ni Mpentekoste Mnazarayo Mbaptisti.” Kwa hiyo, hiyo ni pamoja.

13 Wakati nilipokuja miongoni mwa watu wa Kipentekoste, miaka michache iliyopita, ambayo Bwana alinituma huko, wakati Yeye alipochagua kwamba ninapaswa kuwaombea watoto Wake wagonjwa. Na kanisa lenyewe la kimadhehebu nililokuwa nalo kwenye wakati huo halikuamini sana katika kuwaombea wagonjwa, au uponyaji wa Kiungu. Lilikuwa ni jambo la kigeni kwao. Waliniambia nilikuwa nimefanyika mtakatifu anayejibingirisha. Na vema, labda nimekuwa mtakatifu anayejibingirisha. Sijui. Ila nina furaha sana, chochote nilicho. Na mtu fulani alisema nilikuwa nimerukwa akili. Nikasema, “Basi achana tu na mimi, kwa sababu nina furaha zaidi hivi kuliko nilivyokuwa vile vingine.” Kwa hiyo ni—ninajisikia tu vizuri hivi. Na mimi. . .Imekuwa ni furaha isiyoneneka.

14 Lakini nilipokuja miongoni mwa watu wa Kipentekoste, ni—nilidhani kulikuwa tu na kundi moja la hao. Ndipo basi, nikaja kugundua, karibu yapo tu makundi mengi yaliyojitenga, ndani yao, kama yalivyokuwa katika kanisa la Kibaptisti nililotoka. Basi nisingechukua upande na makundi yoyote. Nilijaribu kusimama kati yao wote na kusema, “Sisi ni ndugu.” Mnaona? Na huo umekuwa mtazamo wangu tangu: kuona kanisa kuu la Mungu aliye hai likiungana pamoja katika imani na maombi na juhudi.

15 Ndipo basi wakati Wafanyabiashara wa Full Gospel walipounda jamii yao, kwa sababu wao si dhehebu. Wao ni jamii. Na hiyo ilichukua katika makundi yote. Basi ilinipa mahali, na wakanichukua chini ya ubawa wao. Nami nina shukrani tele kwa ajili ya fursa ya kuzungumza kwa ajili ya Wafanyabiashara Wakristo, kwa sababu hapo ninaweza kueleza imani yangu miongoni mwa makundi yote kwa wakati mmoja. Na limekuwa ni jambo kubwa kwangu. Basi mimi ni mshiriki wa shirika moja, hilo ni Wafanyabiashara wa Full Gospel.

16 Na kufanya hivyo, ipo sasa katika Afrika, mahali ambapo tunaandaa, kuenda moja kwa moja, huko chini Afrika Kusini, ambapo Bwana alitupatia moja ya mikutano mikubwa zaidi ambao ninafikiri Yeye aliwahi kutupatia, ulikuwa ni chini huko

Afrika Kusini, ambapo tuliona wenyeji elfu thelathini wanaovaa blanketi wakimpokea Kristo kama Mwokozi katika ibada moja ya alasiri. Waliandikisha elfu thelathini.

17 Kesho yake asubuhi, wakati Sidney Smith, meya wa Durban, alinipigia simu, ambaye alikuwa kwenye mkutano. Tulikuwa na yapata watu laki mbili kwenye uwanja, ama ninii—ama uwanja wa mashindano ya mbio. Ndipo akasema, "Nenda kwenye dirisha lako na utazame nje ya dirisha." Ndipo kukaja malori saba yaliyojaa. Na hayo malori makubwa ya Kiingereza yalikuwa kabisa, karibu chumba hiki chote, yamejaa mikongojo na viti vya magurudumu, na—na vitu ambavyo watu walikuwa wamelalia, siku iliyotangulia. Nao walikuwa wanatembea nyuma ya hayo malori, wakiimba, huku wameinua mikono yao hewani, wimbo ambao mliimba dakika chache zilizopita, "Amini tu, mambo yote yawezekana."

18 Nami, moyo wangu, nilisema, "Bwana, hii itakuwa ni siku ya kumbukumbu kwangu mimi." Ndipo siku chache . . . siku ile . . . nilikuwa niwe huko siku tatu pekee. Na huko ndiko ninakorudi tena sasa. Na huko, siku tatu, na si—sijui tu yote yaliyotendeka. Hayo yalifanyika kwa muujiza mmoja tu ambao Bwana alifanya jukwaani; akampa mvulana, aliyekuwa akitembea kwa mikono yake na miguu, kama mbwa, akamrejeshea akili zake timamu na kumnyosha, mbele za watu. Na siku iliyotangulia, watu hao ilibidi watenganishwe kwa uzio kwa sababu walikuwa na vita vya kikabila. Na sasa walikuwa na amani, wakitembea huku wamekumbatiana, wakiimba, "Amini tu, mambo yote yawezekana."

19 Nakwambia, Injili nzuri ya kale, japo katika urahisi wake, haijawahi kupoteza nguvu zake ikihubiriwa katika urahisi wa ufufuo wa Kristo. Na mimi . . . Inazidi kuwa ya thamani kwangu, kila siku.

20 Basi kama wewe ni mfanyabiashara hapa usiku wa leo, na hujaingia katika ushirika wowote wa Wafanyabiashara, hebu mimi nipendekeze hawa Wafanyabiashara wa Full Gospel. Haikulazimu kuwa mfuasi wa kanisa lolote, ama—ama kanisa lolote ulilo ndani yake, ni sawa kabisa. Lina jina "Wafanyabiashara wa Full Gospel." Bali si lazima iwe ni mtu wa full Gospel kufanya hivyo. Wamethodisti, Wabaptisti, Lutheri, Wapresbiteri, hata makasisi wa Katoliki, yeyote yule pale.

21 Mnajua, ninaamini Yakobo alichimba kisima na Wafilisti wakamfukuza kutoka kwacho. Ninaamini alikiita, "uovu," au kitu fulani. Akachimba kingine, wakamtimua kutoka kwa hicho. Akakiita, "ugomvi." Nao wakachimba cha tatu; akasema, "Ipo nafasi kwa ajili yetu sote." Kwa hiyo nafikiri hicho ndicho hiki kilicho; kuna nafasi kwa ajili yetu sote hapa. Nasi tungefurahia kuwa nawe katika eneo hili la Tucson hapa, kuja na kushiriki nasi.

22 Na halafu usisahau mkutano wa Phoenix. Basi sasa, ninajua hatupaswi kutoa tangazo la biashara kutoka jukwaani hapa, maana tumeifanya hiyo kuwa sera. Lakini kwa kuwa haya yote yanahusiana na Wafanyabiashara wa Full Gospel, ninapaswa kuwa na maombi kwa ajili ya wagonjwa, na kuhubiri, siku nne kabla ya mkutano kule Ramada, Desemba hii ijayo... [Mtu fulani anasema, "Januari."—Mh.] Januari ninii... ["tarehe 19 hadi 23."] tarehe 19 hadi 23. Siku nne. Nitaanza tarehe 19, hiyo ni kweli? ["Naam."] Ninaanza tarehe 19. Na ndipo ninakuwa na mkutano, wa siku nne.

23 Na kwenu enyi watu wa Tucson, Jumapili ijayo usiku, ninaombea wagonjwa, huko kwenye Assemblies of God, Grantway, kanisa la Ndugu Arnold Mack. Iwapo kuna mtu mgonjwa na angependa kuja, nitakuwa nikihubiri huko, Bwana akipenda, Jumapili ijayo usiku, nikiwaombea wagonjwa.

24 Na sasa naomba baraka za Mungu zikae juu yenu. Na ikiwa unayo Biblia yako, ningependa kuenda haraka kwenye Neno, kwa sababu ninajua wengi wenu hufanya kazi kesho. Nami nitawazungumzieni usiku wa leo kutoka kwenye Maandiko ambayo ninataka kusoma kutoka kwenye kitabu cha Warumi, Warumi mlango wa 8. Na tunataka kuanzia kwenye kifungu cha 28, na tusome hadi kifungu cha 32, vyote pamoja. Warumi 8:28.

> *Nasi twajua ya kuwa mambo yote hufanya kazi pamoja kwa wema kwa wale wampendao Mungu, kwa wale ambao... walioitwa kwa kusudi lake.*
>
> *Maana wale aliowajua tangu asili, aliwachagua tangu asili wafananishwe na mfano wa Mwana wake, ili yeye awe mzaliwa wa kwanza miongoni mwa ndugu wengi.*
>
> *Na wale aliowachagua tangu asili, hao akawaita; na wale aliowaita, hao akawahesabia haki; na wale aliowahesabia haki, hao akawatukuza.*
>
> *Basi, tuseme nini juu ya hayo? Mungu akiwapo upande wetu, ni nani awezaye kuwa dhidi yetu?*
>
> *Yeye asiyemwachilia Mwana wake mwenyewe, bali alimtoa kwa ajili yetu sisi sote, atakosaje kutukirimia na mambo yote pamoja naye?*

25 Bwana na aongeze baraka Zake kwenye kusomwa kwa Neno Lake. Na sasa ninataka kuzungumza juu ya somo la: *Msamaha*. Biblia ilisema hapa, usiku wa leo, kwamba, "Yeye alitupatia vitu vyote." Vema, hakika hatungeweza kuzungumza juu ya "vitu vyote." Bali tutachukua kitu kimoja ambacho Yeye ametupatia, na hicho ni: *Msamaha*. Nami nafikiri hilo ni neno lenye utukufu, "kusamehewa." Kwa sababu, sisi sote tuna hatia ya dhambi. Sote tumetenda dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu. Basi Mungu, kupitia Mwana Wake, ametusamehe kutokana na hatia hii ya uovu wa dhambi.

26 Na msamaha hunikumbusha kuhusu hadithi niliyosoma wakati mmoja, wa katika Vita vya Mapinduzi, ninaamini ilikuwa. Kwamba, kulikuwa na mtu, askari, askari aendaye kwa miguu ambaye alikuwa amefanya jambo ambalo lilikuwa... Mahakama zilimpata na hatia naye alihukumiwa kupigwa risasi. Ninaamini ndivyo ilivyokuwa, kuacha mahali pake pa kazi katika wakati wa vita. Basi a—alikuwa anaenda kuuawa na kundi la wapiga risasi.

27 Ndipo jamaa mmoja akamhurumia mtu huyu mpaka hatimaye akaenda kwa Ra—Rais mkuu Lincoln. Lincoln, akiwa ni Mkristo mwungwana...Walisema alikuwa akisafiri katika gari lake wakati tarishi alipokutana naye. Ndipo akaanguka magotini mwake na kusema, "Bw. Lincoln, rais wa Marekani, bwana mwenye fadhili," akasema, "ninaomba rehema kwa ajili ya mmoja, nikijua kwamba wewe ni Mkristo, na ninajua kwamba una huruma moyoni mwako kwa ajili ya wanaotaabika." Akasema, "Rafiki yangu alikuwa kwenye mahali pa wajibu alipowekwa, lakini wakati bunduki zilikuwa zinanguruma na mizinga kutupa risasi, aliogopa na kuacha mahali pake pa wajibu. Bw. Lincoln, hakumaanisha kufanya hivyo. Yeye ni mtu mwema. Na sasa, katika juma moja kuanzia leo, hana budi kufa kwa kundi la wapiga risasi. Hakuna njia ya kumwokoa isipokuwa wewe utie sahihi msamaha wake."

28 Bw. Lincoln, akiwa na machozi machoni mwake, alivuta kijipande cha karatasi kutoka kwenye kasha lake na kuandika hapo, "Mimi, Abraham Lincoln, ninamsamehe mtu huyu kwa *hili*, na hatakufa," na akatia sahihi jina lake kwa hilo.

29 Naye mtu huyo akampa baraka za Mungu. Kisha akarudi kwenye gereza, na kumwambia rafiki yake, "Ninao msamaha wako." Ndipo akautoa, juu ya kijipande cha karatasi, na kumwonyesha.

30 Naye mtu huyo akasema, "Usinidhihaki. Hapa ninajiandaa kufa, na halafu unakuja na kama hayo? Siamini hayo. Siwezi kabisa kuamini. Hayo si kweli. Mtu yeyote angeweza kutia sahihi jina lake, 'Abraham Lincoln.'"

31 Akasema, "Lakini hii ni sahihi ya rais." Kasema, "Umesamehewa."

32 Ndipo akageuza mgongo wake na kuondoka. Na mtu huyo akafa chini ya kundi la wapiga risasi.

33 Halafu basi hapa kuna u—u—ufunguzi kutoka kwa Abraham Lincoln, rais wa Marekani, kumwachilia huru mtu huyu, na hata hivyo walimpiga risasi. Kwa hiyo, kesi ikasikilizwa katika Mahakama ya Muungano, na haya hapa yalikuwa ndiyo maamuzi, "Msamaha si msamaha isipokuwa ukubalike kama msamaha."

34 Kwa hiyo hili nililosoma usiku wa leo, kwamba Mungu hutupatia vitu vyote, na Yeye hutupatia msamaha, ni msamaha

kwa wale wanaotaka kulikubali Neno la Mungu kama msamaha. Lakini tu, sisi kulisoma, haimaanishi kwamba umesamehewa. Inamaanisha kwamba inakubidi kuupokea kama msamaha wako, kwamba Mungu alimtoa Mwana Wake kufa badala yako, ndipo basi ni msamaha.

35 Kuwekwa huru na hatia, ndilo ambalo tungependa kuweka juu ya hili. Msamaha kutoka kwa Mungu ni kuwekwa huru na hatia. Si kuondolewa na fundisho fulani la kisaikolojia la aina fulani ambalo kwa namna fulani huenda likakupa hisia ndogo kwamba umefanya kilicho sahihi, kwa kujiunga na kanisa, ama kuchukua kanuni fulani ya imani. Bali ni ku—kuwekwa huru kutoka kwa hatia yako, kwa nguvu za Kalvari. Kitu fulani kimekuweka huru. Hakuna hatia tena. Biblia inasema, ninaamini, katika Warumi 5:1, "Sasa basi hakuna hukumu ya adhabu juu yao walio katika Kristo Yesu, wasioenenda kwa kufuata mambo ya mwili, bali mambo ya Roho."

36 Sasa, mtu, wakati amewekwa huru kutokana na dhambi, mwanamume au mwanamke, hakuna tena shauku ndani ya moyo wao kuenenda kwa kufuata mambo ya ulimwengu. Amesamehewa bure na anakuwa kiumbe kipya ndani ya Kristo Yesu. Na shauku zake ziko kwenye mambo yaliyo juu, ambapo Kristo ameketi katika mkono wa kuume wa Mungu. Amewekwa huru bure. Haimlazimu kuwa na kasisi fulani kumwambia au mhudumu fulani kumwambia. Anajua ndani yake kwamba amesamehewa, kwa sababu ameukubali juu ya misingi kwamba Mungu aliutuma kwake, kupitia Yesu Kristo. Ni hisia ya jinsi gani kuwa huru kutokana na dhambi!

37 Niliambiwa, wakati Kuwekwa huru kwa Tangazo kulipotiwa sahihi kwa ajili ya watumwa kule Kusini, miaka mingi iliyopita, kwamba wakati uliowekwa kwamba walikuwa huru ulikuwa ni kwenye mapambazuko asubuhi fulani. Na wote waliondoka kwenye shamba hilo la kale. Na wengi wa vijana wa kiume walipanda juu kwenye kilele cha mlima, kwa sababu waliweza kuona jua likichomoza kwanza, na halafu wanaume wenye umri mkubwa zaidi, chini kidogo ya hapo, halafu wanawake na watoto sehemu ya chini. Nao walikuwa wanangojea muda mrefu kabla ya mapambazuko. Maana, kanda za utumwa, majaribu makali yalikuwa yametia alama maisha yao kwa huzuni, nao walitamani siku hiyo ambapo kwamba walijua kwamba walisamehewa. Nalo Tangazo la Uhuru lilisema, "Katika siku hii fulani, kwenye mapambazuko, wako huru." Basi walikuwa wanatamani kuiona saa hiyo ambapo jua lilichomoza, kwa hamu sana hata wakapanda milima.

38 Loo, laiti wenye dhambi usiku wa leo wangeweza tu kuwa na hamu kiasi hicho kujua kwamba umesamehewa. Umesamehewa dakika ile ambayo unamkubali Yesu Kristo kama Mwokozi wako. Ndipo umesamehewa.

39 Walisema kwamba vijana wa kiume walingojea. Na punde tu jua lilipoanza kuangaza mashariki, waliwapigia mayowe wenye umri mkubwa zaidi waliokuwa chini, "Tuko huru!" Na wenye umri mkubwa chini, kwa wanawake na watoto, "Tuko huru! Tuko huru!" Kwa sababu jua lilichomoza.

40 Loo, wakati mwanadamu alikuwa amejiuza kwa dhambi, na wakati Mwana wa Mungu alipoinuka kutoka kaburini asubuhi ile, kwa ajili ya kutuhesabia haki, nafikiri inapaswa kuwa ni mayowe kote katika mataifa, "Tuko huru kutokana na dhambi na aibu, tumesamehewa bure kwa vifungo vya Kalvari." Hakuna kitu kikuu zaidi ambacho kingeweza kutolewa kwa jamii ya wanadamu.

41 Wakati mwanadamu alipotenda dhambi katika Bustani ya Edeni, alivuka shimo kubwa, akijitenga mwenyewe kutoka kwa Yule wa Milele. Mwanadamu wakati huo alikuwa wa Milele pamoja na Mungu. Hakuwa na ugonjwa wowote, huzuni, au mauti. Mwanadamu hakuumbwa ili afe. Kuzimu hakukufanywa kwa ajili ya mwanadamu. Kuzimu kuliumbwa kwa ajili ya ibilisi na malaika wake, na si kwa ajili ya mwanadamu. Kwa sababu, waliumbwa duniani ili kuwa wana na binti za Mungu. Lakini wakati mwanadamu alipotenda dhambi na kuvuka mstari wa mpaka kati ya mema na mabaya, alijitenganisha mwenyewe kutoka kwa Mungu, akijiacha mwenyewe bila njia ya kurudi. Alikuwa amepotea kabisa. Hangeweza kurudi, kwa sababu alikuwa ametenda dhambi.

42 Lakini, Mungu, aliye mwingi wa rehema, alikubali kibadala. Kwa sababu Yeye alikuwa amesema, "Siku utakayokula kutoka hapo, siku hiyo utakufa." Nayo haki ya Mungu na utakatifu Wake huhitaji kifo, kwa sababu ni Neno Lake. Na Yeye hana budi kutimiza Neno Lake, ili awe Mungu.

43 Na sasa, upendo ambao Yeye alikuwa nao kwa jamii ya wanadamu, na hata hivyo ilimbidi kuwaona wametengwa kutoka Kwake, na ushirika ambao Yeye alikuwa nao pamoja na watoto Wake katika bustani ya Edeni, katika hali hiyo ya kuvunjika moyo ambayo ilimbidi Yeye kuwa katika wakati huo wote, kwa sababu Neno Lake lilisema, "Siku utakayokula, siku hiyo utakufa."

44 Basi, tunaweza kuegemea kwenye hili, lolote asemalo Mungu ni kweli. Halina budi kutimia. Mungu hawezi kulighairi Neno Lake, unaona, kwa sababu Yeye hana kikomo, na Yeye ni wa Milele. Na uamuzi Wake wa kwanza ni uamuzi wa wakati wote. Haimbidi Yeye ku—kulighairi kwa sababu Yeye amejifunza zaidi juu yake. Yeye hana kikomo, kwa kuanzia. Na kwa hiyo, wakati Mungu anaposema chochote, ni hivyo kikamilifu. Hakiwezi kubadilishwa, kwa sababu ni uamuzi mkamilifu.

45 Na halafu jinsi Mungu hutenda juu ya wa—watu ambao wanakubali uamuzi Wake, daima itatenda juu ya kila mmoja

ambaye anaukubali uamuzi Wake namna hiyo. Hivyo basi, kama Yeye alifanya njia kwa mwanadamu kuokolewa, njia ya kwanza ambayo Yeye alifanya daima imebaki vivyo hivyo. Na ikiwa Mungu aliahidi uponyaji kwa wagonjwa, juu ya msingi wa imani ya kuuamini, daima inabaki hivyo. Hawezi kulighairi. Unaona? Yeye lazima abaki vivyo hivyo daima.

46 Sasa, Mungu alikubali kibadala kwa ajili ya mwanadamu katika bustani ya Edeni, na hiyo ilikuwa ni njia ya sadaka ya damu. Damu ilibidi ilipe gharama. Na daima imekuwa hivyo. Hakujawahi kuwa na njia yoyote nyingine, au kitu chochote kingine, kilichowahi kuchukua mahali pake. Ilikuwa ni damu. Njia ya pekee ambayo Mungu hupokea watoto Wake kurudi, ni kwa kibadala hiki cha damu. Hakuna gharama yoyote nyingine iwezayo kulipwa. Hakuna chochote kingine kitakachofaulu. Uamuzi wa kwanza wa Mungu daima ni mkamilifu, na ni wa Milele. Na sisi tunajua kuwa hiyo ni kweli, kwa sababu Mungu hawezi kusema uwongo, pia Yeye hawezi kughairi Neno Lake. Tangu wakati huo, imekuwa ndiyo njia ya pekee ya Mungu na mahali pekee pa ushirika na mwanadamu. Sasa, somo lilikuwa . . .

47 Sasa, neno *kifo* linamaanisha "utengano." Tunapokufa kwa njia hii, haimaanishi . . . Kifo chetu cha kimwili hakimaanishi kwamba tumekufa. Yesu alisema, "Yeye aniaminiye Mimi, ajapokufa, hata hivyo ataishi. Yeyote aishiye na kuniamini Mimi hatakufa kamwe." Sasa, hicho *kifo,* anachozungumzia hapo, ni "utengano" kutoka Uweponi mwa Mungu. Lakini kifo cha kimwili ambacho kinatubidi kupitia hapa, hata hivyo si kifo. Tungali katika Uwepo wa Mungu. Tunasonga kutoka mahali hapa hadi mahali karibu zaidi na Yeye, katika Uwepo Wake. Si kifo kile tunachokiita "kifo," tunachokiita hapa.

48 Kumbukeni, Yeye alisema kwa yu—yule msichana aliyekufa, binti wa Yairo, "Hajafa, bali analala."

49 Nao wakamcheka Yeye na kumdhihaki, Yeye, wakijua kwamba huyo alikuwa amekufa. Hilo ni tamshi lao, "Alikuwa amekufa."

50 Bali Yesu alisema, "Analala." Ndipo Yeye akaenda na kumwamsha, naye akarudi kuwa hai.

51 Sasa, kuanzia Adamu hadi sasa, mwanadamu amejaribu kutengeneza kibadala chake mwenyewe. Amejaribu awezavyo kufanya jambo bora kidogo zaidi ya kile Mungu alicholifanya wakati ule. Na hiyo tu ni kawaida kwa mwanadamu. Mwanadamu daima anajaribu ku—kuboresha kitu fulani, kukifanya vinginevyo. Anataka kuingiza mawazo yake mwenyewe katika mpango wa Mungu. Na hiyo ndiyo sababu tunasimama usiku wa leo tumetengana, watu Wakristo wa ulimwenguni, kwa vizuizi, kwa vizuizi vya kidhehebu. Sisi . . . Inafanya hivi kwa sababu mwanadamu ameingiza mawazo yake

mwenyewe katika mpango wa Mungu. Tangu Adamu hadi sasa, kama nilivyosema, imekuwa hivyo.

52 Adamu alidhihirisha mawazo ya mwanadamu, katika bustani ya Edeni, wakati alipojitengenezea nguo ya jani la mtini ili kumkabili Mungu. Ni jambo ambalo alifanya, mwenyewe. Na kutoka kwenye majani ya mtini, amejaribu elimu, minara, majiji, sanamu, ustaarabu, dhehebu. Lakini inabaki vile vile. Mungu huwakubali tu watu Wake chini ya Damu. Hayo tu.

53 Elimu imeshindwa kabisa. Kadiri tunavyozidi kupata elimu, ndivyo tunavyozidi kwenda mbali mmoja na mwenzake. Dhehebu limeshindwa kabisa. Tunachora mipaka na vizuizi, na kila mmoja akijaribu kulifanya dhehebu hilo kuwa juu kuliko jingine, na hilo huvunja ushirika. Ustaarabu umeleta tu mchafuko. Majiji, minara, na chochote zaidi, vimeshindwa vyote. Nao mpango wa Mungu ungali unabaki vile vile: chini ya Damu.

Damu hii haina budi kuwa ni damu iliyowekwa wazi. Katika bustani . . .

54 Huko nyuma katika wakati, hasa, wa Israeli, wakati Israeli ilipowabidi kumwua mwana-kondoo na kuweka damu juu ya kizingiti na juu ya mwimo wa mlango, Mungu alihitaji hiyo. Na ishara hiyo lazima iwepo hapo, haijalishi ni msimamo upi mwingine. Wanaume hao huenda waliweza kuonyesha kwamba walikuwa Waisraeli waliotahiriwa. Huenda walikiri kwamba, "Sisi tunaamini kila neno ambalo Yehova anasema." Lakini hilo halikuiondoa. Ilibidi waiweke wazi ishara hiyo. Damu haina budi kuonyeshwa.

55 Hivyo ndivyo ilivyo usiku wa leo. Ninaamini kwamba kila Mkristo hana budi kuweka wazi Damu ya Yesu Kristo ambayo imewatakasa kutokana na mambo ya ulimwengu, haidhuru.

56 Sasa, katika wakati huo, ishara sharti iwe mlangoni. Lazima iwepo, haijalishi jinsi nyumba hiyo ilivyokuwa ya kidini, jinsi watu walivyo wa kidini, jinsi walivyokuwa wamewalea watoto wao vizuri, jinsi walivyohudhuria kanisa vizuri, jinsi walivyokuwa wameweka wazi vizuri vitu vyote ambavyo Mungu alisema. Ingali, kwenye saa ile ya mwisho, mahali ilipoonyesha kati ya mauti na uzima, ilibidi damu iwekwe wazi. Nayo damu ilionyesha kwamba kibadala kisicho na hatia kilikuwa kimechukuliwa kwa niaba ya mwabuduo. Nayo kemia ya damu, damu nyekundu yenyewe, ilikuwa ni ishara juu ya mlango kwamba nyumba hii ilikuwa salama, chini ya damu. Sasa, huo ulikuwa ni mfano.

57 Sasa, katika siku hizi za mwisho, tunarudi tena kwenye saa ya Mungu kulikomboa Kanisa Lake. Ni—ninaamini hilo. Na kwa hakika kama ilivyobidi damu ile isimame kama kumbukumbu, vivyo hivyo na ishara inabidi iwe. Inahitajika leo hii. Kwa kuwa, sasa, wasingeweza kuchukua kemia ya Damu ya Bwana Yesu na kuiweka juu ya mlango wa kila moyo.

58 Bali, unaona, wakati huo, mnyama alikufa, ambaye alikuwa ni mwana-kondoo. Na ili kuonyesha kwamba mnyama alikufa, damu ilikuwa juu ya mlango. Kwa hiyo uhai uliokuwamo ndani ya huyo mnyama haungeweza kuja juu ya mwabuduo, kwa sababu mnyama hana nafsi. Kwa hiyo uhai uliokuwa ndani ya mnyama haungeweza kuja juu ya mwabuduo.

59 Lakini, leo hii, wakati Damu ya Mwana wa Mungu mwenyewe ilimwagwa pale Kalvari kwa ajili ya msamaha na uhuru wetu, uhai uliokuwa ndani ya hiyo Damu ulikuwa ni Mungu Mwenyewe. Ndipo Roho Mtakatifu anarudi juu ya Kanisa Lake, juu ya mwaminio Wake, na ni ishara katika siku hizi za mwisho, kwamba Yeye atapita juu ya mwanaume au mwanamke ambaye amekubali kifo cha Yesu Kristo kama kibadala chao. Na Roho Mtakatifu anashuhudia.

60 Huenda ukasema, "Nimemkubali Huyo." Na ungali unaishi katika ulimwengu, ungali unaishi kama ulimwengu, basi hakuna ushahidi kwamba Uzima huo ulikuwa kwa ajili yako, mpaka ushahidi huo wa Roho Mtakatifu umeingia ndani ya maisha yako.

61 Hilo hapo hitaji la Mungu, ambalo kila mwanaume au mwanamke hana budi kuwa nalo, ushahidi huo kama ishara katika siku hii ya mwisho. "Nionapo Damu."

62 Yesu alisema, "Amin, amin, nawaambia, mtu asipozaliwa mara ya pili, kwa maji na Roho, kamwe hataingia katika Ufalme."

Hivyo basi umekuwa ni mpango wa Mungu, wakati wote, Damu. Ilikuwa damu katika Agano la Kale. Ilikuwa Damu katika Agano Jipya.

63 Katika Agano la Kale ilikuwa ni kemia, ambayo ilikuwa ni mfano wa uhai unaopaswa kuja. Ilionyesha kwamba kulikuwa na kibadala kilichochukuliwa, lakini mwabuduo alitoka na dhamira ile ile ya hatia aliyokuwa nayo wakati alipoingia na kumtoa mwana-kondoo wake.

64 Lakini kwa njia hii, "Wakati mwabuduo, akishakutakaswa kutokana na dhambi, hana tena dhamira yake," kitu hicho kimekufa, kimetoweka, nawe umebadilika kutoka mautini kuingia Uzimani. Na wewe uko hai tena ndani ya Kristo Yesu pamoja na Uzima wa Milele, Roho Mtakatifu akitulia ndani yako, akileta Uzima wa Yesu Kristo tena. Kwa kuwa Biblia ilisema, katika Waebrania 13:8, "Ni yeye yule jana, leo, na hata milele."

65 Mungu anangojea saa kuona Kanisa Lake likija mahali hapo, pasipo kujali dhehebu, pasipo kujali kanuni ya imani, rangi, au chochote kiwezacho kuwa, hata Kanisa Lake lote litafikia mahali ambapo wanaonyesha ishara ya kifo cha Yesu Kristo.

66 "Kwa kitambo kidogo," Yeye alisema, "na ulimwengu hautaniona Mimi tena, hata hivyo nyinyi mtaniona Mimi; kwa sababu ninaishi, mnaishi pia. Nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hadi mwisho wa ulimwengu," Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele.

67 Ninakuta miongoni mwa Wakristo wakati mwingine wale wanaodai kuwa wanaume watakatifu, wanawake wa Mungu. Wanaonea aibu ushuhuda. Wanaona aibu kusema, "Amina." Wanaona aibu kuimba nyimbo za Sayuni. Wanaona aibu kila mahali. Ninapenda kuwa miongoni mwa watu ambao hawaaibikii Injili ya Yesu Kristo. Ingawa Hiyo inaonekana kama uzushi, lakini hata hivyo hawaaibiki. Jambo fulani limetukia, na Hiyo inamaanisha zaidi ya uhai kwao. Ni uzima. Ni Uzima wa Milele kwa sababu wamekubali kibadala cha Mungu.

68 Ninapenda uimbaji wa namna hii. Nilipokuwa huko nyuma nikiwaombea watu fulani, dakika chache zilizopita, ambao walikuwa wameletwa ndani. Na hii ikiwa si ibada ya maombi; kuzungumza tu. Nilikuwa humo ndani. Na ningeweza kuzisikia nyimbo, kupiga makofi kwao. Na sisi tunashangaa . . . Na baadhi yao hata, niliwaona, wakikimbia huku na huku sakafuni, kile wanachokiita "kucheza katika Roho."

69 Mwanzoni, nilikuwa mkosoaji wa hilo, nilipowaona watu wa Kipentekoste wakicheza katika Roho. Nami nikawazia, "Ni nini hili? Lazima ni kundi la upuuzi." Ndipo nikaanza kusoma Biblia, na nikapata, kwamba, huku wakicheza katika Roho. Ibilisi aliiga hiyo na kuwaweka huko nje pamoja na roki na upuuzi, lakini dansi ya kweli halisi ilitoka kwa Mungu. Hiyo ni hakika. Na, daima, dansi ilikuwa ni ushindi.

70 Wakati Daudi alipomwua Goliathi, na maskini mvulana huyu aliyeonekana mwekundu akaja akivuta kichwa cha jitu hili akiingia jijini, watu walikutana naye, wakicheza. Walikuwa na ushindi. Wakati Musa alipovuka Bahari ya Shamu, kwa uwezo wa Mungu, na kuwapeleka watoto wa Israeli upande ule mwingine, Miriamu alichukua tari, na binti wote wa Israeli, na huku na huku ukingoni walienda, wakipiga tari na kucheza katika Roho. Kama huo si mkutano wa kale wa Kipentekoste, sijawahi kuona mmoja maishani mwangu. Shida ilikuwa, kwangu mimi, sikuwa na ushindi wa kutosha. Lakini wakati hatimaye unapopata ushindi huo, nayo ishara ya Damu ya Yesu Kristo inakuja juu yako.

71 Ninamkumbuka Daudi, mtunzi mashuhuri wa zaburi wa Biblia. Wakati alipokuwa amefanya jambo, ambalo, hili jambo kuu, alipewa binti wa Sauli. Naye kwa namna fulani alikuwa aliyedhaniwa kuwa mwaminio, wa mtindo wa kibinafsi, mwenye mtindo wa kibinafsi. Na sanduku lilishakuwa mbali na Mungu kwa muda mrefu, Uwepo wa Mungu unaoonekana, Nguzo ya Moto ikining'inia juu ya sanduku hili. Wafilisti walikuwa

wameingia na kulichukua chini ya utawala wa Sauli. Ndipo siku moja, wakati Daudi alipoona sanduku likirudi kwenye nyumba ya Mungu, Daudi alienda mbio mbele ya sanduku, na akacheza mbele za Bwana, akiimba sifa za Mungu. Naye binti ya Sauli alionekana kuaibika sana na matendo ya mtu huyo. Mume wake, mume wake, kijana mwenye sura nzuri alikuwa amemwudhi na kutenda yasiyofaa mbele zake, binti ya mfalme. Ndipo Daudi akasema, mengi sana, "Ikiwa hupendi hilo, tazama hili kwa kitambo." Na akazunguka, na kuzunguka, na kuzunguka sanduku tena, akicheza katika Roho. Naye mwanamke huyo akaaibika. Ndipo Mungu akamlaani huyo mwanamke kwa laana.

72 Loo, ushindi kupitia Damu ya Yesu Kristo, ishara ya ufufuo wa Kristo, maisha Yake yanaishi ndani ya Kanisa Lake. Hakuna njia nyingine ya ushirika, chini, ila chini ya hiyo Damu. Madhehebu yetu yatatutenganisha, na mmoja anasema, "Huo ni upuuzi." Na mwingine anasema *hili*, *lile*, ama *linginelo*.

73 Pentekoste ilikuwa mfano wetu. Hakuna mtu atakayesema ila kile . . . ama anaweza kusema ila kwamba Kanisa lilianzishwa kwenye Siku ya Pentekoste. Na Roho yule yule aliyekuja juu yao kwenye siku ile, kila mara bila kukosea, katika Biblia, wakati Roho Mtakatifu alipokuja juu ya watu, walitenda vile vile.

74 Hebu niseme hili, kwamba katika nchi za makafiri ambapo nimekuwa na mahali, majaliwa ya kusafiri na kuwaona wenyeji wavaao blanketi wa visiwani na katika Wahotentoti, na kuwaona wakisimama hapo ambapo inakubidi kuzungumza kupitia mkalimani, hawakuwahi kusikia Jina la Yesu Kristo katika maisha yao. Lakini hebu wasimulie Hadithi hiyo, na uwaulize kuinua mikono yao na kumpokea Mungu, wanafanya jambo lile lile mnalofanya papa hapa wakati mkimpokea Roho Mtakatifu. Inaonyesha kwamba ni jambo la kila mahali. Ni nguvu za Mungu Mwenyezi, onyesho la ishara Yake juu ya watoto Wake, wawe ni wekundu, weusi, weupe, ama chochote wawezacho kuwa. Ndipo mahali pa pekee ambapo ushirika umetolewa.

75 Nimrodi alijenga mnara, naye Nubkadreza mji, na kadhalika. Wanaendelea kote kupitia wanasayansi na kila kitu, lakini ingali inabakia kwamba ilikuwa ni damu. Hapo, Mungu alifanya uamuzi Wake kwamba ingekuwa ni kibadala kisicho na hatia, kingebidi kichukue mahali pa mtu aliye na hatia kwa ajili ya msamaha, na inabaki kitu hicho hicho usiku wa leo, na kamwe hajabadilisha hicho.

76 Ayubu aliishi kwa hicho. Ayubu, kitabu cha kale kuliko vyote katika Biblia. Ingawa mambo yote yalimtokea mtu huyo, hata hivyo alisimama imara kwa sababu alijua alikuwa ametimiza matakwa ya Yehova. Alijua ilikuwa sahihi. Ibrahimu, vivyo hivyo; wengi wao. Israeli ilikutana tu . . . Kulikuwa na mahali pamoja tu ambapo Israeli iliweza kuwa na ushirika:

hapo palikuwa ni chini ya damu iliyomwagika. "Wanadamu wanapaswa, kila mahali, kuabudu katika Yerusalemu." Hadi kulipokuwa na dhabihu, hapakuwepo ibada. Nayo dhabihu ilikuwa damu.

77 Leo, leo, pamoja na kuelimishwa kabisa kama taifa linavyoonekana kuwa, na waliostaarabika kama wanavyoonekana kuwa, na utafiti wetu wote wa kisayansi kupasua atomu, na chochote kinachotendeka, kurusha roketi kwenye mwezi, ama kutuma sa—sateliti, ama chochote kiwezacho kuwa. Utafiti wetu wote wa kisayansi, madhehebu yetu yote, elimu yetu yote, shule zetu zote, zimetupeleka tu mbali na Mungu kuliko zilivyokuwa mwanzoni.

78 Kinachohitajika ni moyo uliosalimishwa kwa nguvu za Mungu Mwenyezi kwa mapenzi Yake, naye Roho Mtakatifu atakuja kama ishara juu ya mtu huyo. "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio." Daima inabaki vile vile. Kristo alisema hivyo. "Enendeni ulimwenguni kote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe. Yeye aaminiye na kubatizwa ataokolewa; yeye asiyeamini atahukumiwa. Na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio." Ni madhihirisho ya Roho Mtakatifu, kwamba Mungu amemkubali mwabuduo, kwa kuwa Roho na Uhai uliokuwa ndani ya Kristo huja juu ya mwabuduo.

79 Hivi waweza kuwazia Myahudi katika siku za kale, chini ya damu iliyomwagika? Huyu hapa anakuja, chini barabarani. Ni—ni siku ya upatanisho. Anaenda kutoa dhabihu. Anaye fahali mzuri, aliyenona. Hilo ni hitaji la Yehova. Au labda tungeweza kusema anaye mwa—mwana-kondoo, mwana-kondoo mzuri, aliyenona. Anaenda kuchunguzwa, na kuhani, kuona ikiwa kuna dosari juu yake.

80 Ndipo basi anaenda mahali pa ibada. Anatambua kwamba yeye ni mwenye dhambi. Amefanya kosa. Sasa, anaweka mikono yake juu ya dhabihu hii. Kwa kuweka mikono yake juu ya dhabihu, anajitambulisha mwenyewe na dhabihu yake. Ndipo basi wakati koo lake linapokatwa, ama uhai wake unapoondolewa; mikono yake ikiwa juu yake, na uhai wake umeondolewa, naye anahisi uchungu wakati mnyama huyo anapokufa, na damu ikirashiwa juu ya mikono yake. Anatambua kwamba mnyama huyo anachukua mahali pake. Naye hapo anarudi, amehesabiwa haki, kwa sababu amefanya hasa kile Yehova alimhitaji kufanya.

81 Na hilo ndilo jambo lile lile lililo na Wakristo leo hii. Si kutia sahihi kadi fulani, kwamba utahudhuria shule ya Jumapili idadi fulani ya siku ama idadi fulani ya Jumapili katika mwaka. Si kuchukua kiapo kwamba hutakunywa tena kwa miezi sita. Si hilo. Ni kuweka mikono yako juu ya Dhabihu ya Mungu iliyotolewa, msamaha Wake, kichwa cha Yesu Kristo, na kuhisi machozi ya kimwili pale Kalvari. Na halafu kujitambulisha

mwenyewe pamoja na Yeye katika ubatizo, ili, kama Yeye alivyokufa na kufufuka tena, ndivyo na wewe unazikwa katika Jina Lake, kufufuka kwa maisha mapya, kutembea kama kiumbe kipya katika Kristo, unapofanya hivyo kwa unyofu.

82 Amefanya hili, agizo la Yehova, na kwa hiyo anajihisi amehesabiwa haki. Sasa, Myahudi angeweza kuhesabiwa haki kwa sababu alikuwa amefanya kile Yehova alimwagiza kufanya. Hatimaye...Hiyo ilikuwa sahihi. Yehova alifanya hilo, na hilo ndilo ambalo Yeye alihitaji. Bali, hatimaye, hilo likawa desturi ya familia. Ikaja siku ya upatanisho na labda Wayahudi walikuwa wanafanya kosa. Angesema, "Vema, ninaamini ni siku ya upatanisho. Afadhali nimpeleke mwana-kondoo wangu huko chini." Unaona, ikawa desturi ya familia. Hawakuenda nalo pamoja na unyofu. Walifanya tu kwa sababu familia zilikuwa zimelifanya. "Hilo ni ja—jambo tu litupasalo kufanya. Familia zote zinalifanya, kwa hiyo tunapaswa kulifanya, pia."

83 Na hapo hasa ndipo ambapo Ukristo wetu umefikia. Hapo ndipo hasa ambapo huduma zetu za Kipentekoste zinafikia. Ni desturi ya familia. Unaona? Hatu—hatujitambulishi wenyewe na Dhabihu yetu, kwamba tumekufa na Dhabihu yetu. Sisi ni...Tunasema, "Loo, sisi ni Wakristo kwa sababu nilienda na kujiunga na kanisa." Kujiunga na kanisa ni sawa. Lakini mpaka utambulishwe, mpaka uweke mikono yako juu Yake, na wewe na Yeye mwe Mmoja, mpaka Roho wa Kristo awe ndani yako, na wewe ndani ya Kristo, mpaka utakapofanyika mwana na binti wa Mungu, hakuonekani kuwepo na unyofu ambao wa—wanapaswa kuwa nao. Inakuwa ni desturi ya ibada. Sawa tu na ilivyo sasa, ni desturi kwa watu kuwa Mkristo.

84 Hapa wakati fulani uliopita nilimwuliza msichana fulani katika mstari wa maombi, "Je! wewe ni Mkristo?"

85 Akasema, "Vema, mimi ni Mmarekani, nitakufanya uelewe." Sasa, kana kwamba hilo lilikuwa na uhusiano wowote nalo.

86 Mmarekani, ni jambo kuu kuwa Mmarekani, lakini hilo halimaanishi wewe ni Mkristo. Huna budi kuzaliwa tena.

Mwanamke mwingine nilimwuliza, "Je! wewe ni Mkristo?"

87 Mbona, alikuwa amechukizwa sana, akasema, "Nakupa ufahamu, mimi huwasha mshumaa kila usiku." Kana kwamba hilo lilikuwa na uhusiano wowote nalo.

88 Huna budi kutambulishwa na Kristo, na Maisha Yake yakiishi ndani yako. Hapo ndipo unatambulishwa na Kristo, ni wakati Kristo anapoishi ndani yako. Si desturi. Si kuwa mshiriki wa kanisa. Hayo yote ni mema, lakini wewe ona unyofu halisi.

89 Wakati tukifikia ibada za uponyaji, kama utatambua kwenye utambuzi mstarini, daima ni, "Waambie watu watubu." Unaona? Hapo unaenda, mpaka maombi yetu yamekuwa desturi. Tunapiga magoti usiku na kusema, "Bwana, mbariki *Fulani-*

*wa-fulani*, na umbariki *Fulani-wa-fulani*, na ufanye *hili*. Na umsaidie John afanye *haya* yote." Unamfanya Mungu ki—kitu cha kubahatishia mambo mazuri, ama unamfanya Yeye na—namna fulani ya mvulana tarishi. "Mungu, Wewe fanya *hili*. Na Wewe fanya *hili*. Na Wewe fanya *hili*." Hivyo sivyo ambavyo Yesu alituambia tuombe.

90 Yeye alisema tuombe namna hii, "Baba yetu uliye Mbinguni, Jina Lako litukuzwe. Ufalme Wako uje. Mapenzi Yako yafanyike duniani, kama yalivyo Mbinguni."

Lakini sisi tunajaribu kumwagiza Mungu, jambo la kutufanyia.

91 Na hiyo ndiyo sababu kanisa linaingia baridi. Hiyo ndiyo sababu uamsho mkuu ambao ndiyo kwanza uingie nchini, umeingiza mamilioni kanisani. Ni, huo, wamefikia mahali ambapo wanatumia matukio haya, na kadhalika, kama desturi, badala ya kuwa na majuto ya kitauwa, na kumwacha Roho Mtakatifu afanye kazi ya ofisi Yake ndani yako, na kuumba ndani yako maisha mapya, na kukufanya mwenye njaa sana kuenda kanisani hata huwezi kukaa mbali na kanisa. Halafu, hilo ndilo lililo. Si kutia sahihi tikiti, na kujiunga, na kuwa na kadhalika. Ni kuwa na Uhai wa Kristo ndani yako, hata unatamani tu kuenda. Kuna Kitu ndani yako, kinachokusukuma.

92 Kama nilivyokuwa nikimwambia kijana fulani hapo jana, katika maongezi, usaili kidogo. Nilisema, "Nilizoea kupitia karibu na chemichemi ndogo, wakati nilipokuwa bwana nyama huko Indiana. Na kulikuwa na . . . "

93 Ilikuwa ndiyo chemichemi yenye furaha kuliko zote niliyowahi kuona maishani mwangu. Chemichemi kubwa katika Indiana, hububujika na hayo maji mazuri baridi, ya maji ya chokaa. Basi siku moja niliketi chini karibu na hiyo chemchemi, kuzungumza nayo, kama tu ninavyodhania kwamba Musa angeketi, kwenye kichaka kilichowaka moto, kuongea nacho. Ndipo nikasema, "Maskini chemchemi, ni kitu gani hukufanya mwenye furaha hivi, hata unabubujika wakati wote? Nikija hapa wakati wa baridi kali, unabubujika. Nikija majira ya kipupwe, majira ya kupukutika, majira ya joto, wakati wowote ule, unabubujika. Je! ni kwa sababu kwamba labda, pengine, una furaha sana kwamba sungura huja na kunywa kutoka kwako?"

94 Vema, sasa, kama angeweza kuongea, angesema, "La, hilo—hilo silo."

95 Ningesema, "Vema, labda kwa sababu kulungu huja na kunywa kutoka kwako."

Angesema, "La, hilo silo."

96 Ningesema, “Sasa, vema, labda ni kwa sababu mimi huja, mara moja moja, na kunywa kutoka kwako.”

97 “La, hilo silo. Nina furaha kwamba wote huja na kunywa, lakini hiyo siyo sababu kwamba ninabubujika wakati wote.”

98 “Vema, ni kitu gani kinachokufanya kububujika namna hiyo? Ni nini kinachokufanya kuwa na furaha sana, daima ukibubujika?”

99 Kama angeweza kuongea, angesema, “Si mimi. Ni kitu fulani nyuma yangu, kinanisukuma.”

100 Hivyo ndivyo ilivyo na ujuzi wa Mkristo. Si kitu fulani ambacho unajaribu kufanyiza. Ni kitu fulani nyuma, kikifanya kazi ndani yako. Ni uzima wa milele unaosonga, ukibubujika. Kama vile Yeye alivyomwambia yule mwanamke kisimani, “Itakuwa ni visima vya maji vikibubujika kuingia Uzima wa Milele.” Ni kitu fulani ndani ya mwabudu wakati ametambulishwa na Kristo, kwa sababu anajua kwamba Yeye yu hai. Bali hatutaki iwe desturi.

101 Israeli ilipofikia mahali ambapo walizifanya amri za Mungu, pamoja na dhabihu zao, desturi, ilikuwa ni hapo ambapo nabii mwenye nguvu Isaya alitumwa na Mungu, kwao, akiwa na BWANA ASEMA HIVI. Mahali fulani, kwa njia fulani, Mungu daima anaweza kuweka mkono wake juu ya mtu ambaye haogopi kurarua kitu kilicho sahihi, mahali fulani, sehemu fulani. Isaya aliinuka, kama utasoma Isaya 1. Nimeandika hapa. Isaya aliwaambia, kasema, “Sadaka zenu ambazo Yehova alihitaji zimekuwa uvundo puani mwangu. Ninazichukia.” Na mafuta ya kondoo dume na—na ya ndama, na kadhalika, Mungu aliyachukia, kitu chenyewe hasa ambacho Yeye aliwaagiza kufanya. Kwa sababu walikifanya kuwa desturi ya ibada, ndipo Mungu akachukizwa nacho, kwa sababu walikifanya desturi ya ibada.

102 Nasi tunaweza kulifanya Neno la Mungu kitu hicho hicho, kweli, wakati tunapolijia kama desturi, kama desturi ya ibada. Hatuna budi kulijia, tukijua ni “BWANA ASEMA HIVI.” Kama Mungu aliliahidi, Mungu atasimama na ahadi Yake. Yeye ni mkubwa kuliko ahadi Yake. Daima amekuwa hivyo. “Yeye anaweza,” kama Ibrahimu alivyosema, “kutimiza kile Yeye alichoahidi kufanya.” Daima anaweza kufanya hivyo, kutimiza Neno Lake.

103 Sasa Isaya aliwaambia, kasema, mambo haya yote ambayo walikuwa wanafanya, walikuwa wamelifanya bila unyofu. Walikuwa wamelifanya kwa sababu tu wale wengine walikuwa wanalifanya. Walikuwa kwa sababu. . .kufanya hilo pia kwa sababu lilikuwa ni hitaji la Yehova. Na familia yote ilifanya hilo, na kina mama walililifanya, na mababu walililifanya. Ni kwa nini hawakuweza kulifanya?

104 Sasa, tunafanya jambo lile lile. "Babu yangu alikuwa Mpresbiteri, kwa hiyo mimi ni Mpresbiteri. Baba yangu alikuwa Mbaptisti, kwa hiyo mimi ni Mbaptisti," na kadhalika. "Na baba yangu alikuwa Mpentekoste, kwa hiyo mimi ni Mpentekoste." Hilo silo.

105 Tunafikia mahali ambapo tunatambua kwamba tumetenganishwa. Tumetenganishwa na Mungu. Basi tunakuja juu ya msingi wa Damu iliyomwagika ya Yesu Kristo. Chini ya Damu hiyo, hapo ndipo Methodisti, Baptisti, Lutheri, Presbiteri, Pentekoste, wote wanaweza kukutana juu ya misingi sawa. Pasipo kujali desturi, wao, au desturi ya ibada, wanaweza kukutana hapo chini ya kitu kimoja shirika, na hicho ni juu ya Damu ya Yesu Kristo.

106 Mpaka kanisa litakaporudi mahali, na mbali na desturi zake za ibada, na kurudi kwenye mpango asilia wa Mungu, hata watu wanazaliwa katika Ufalme wa Mungu na si kujiunga na Kanisa. Hapo ndipo wakati ambapo Ushirika utatamalaki kila mahali. Naye Roho wa Bwana atafunika dunia, "kama maji yafunikavyo bahari," ikifikia mahali ambapo watu wanaweza kusahau tofauti zao na kuja pamoja katika ushirika chini ya Damu. Hatuwezi sote kuja chini ya desturi ya Kibaptisti, ama desturi ya Kipresbiteri, ama chini ya desturi ya Kimethodisti, chini ya desturi ya Kipentekoste. Lakini sote tunaweza kukutana na kushirikiana chini ya Damu ya Yesu Kristo, kwa sababu ni mpango asili wa Mungu. Hiyo ni kweli. Amina. Huo hapo msamaha.

107 Mmethodisti anaweza kumwangalia Mbaptisti na kugeuza kichwa chake kando, naye Mbaptisti anaweza kumwangalia Mpentekoste, na Mpentekoste huko nyuma katika Baptisti, juu ya desturi zao. Bali wanapokutana chini ya msalaba ambapo Damu ya Yesu Kristo husafisha watu wote kutokana na dhambi, yeye ni kiumbe kipya katika Kristo Yesu. Yeye ni ndugu. Haijalishi ni kibandiko gani alichobandikwa nacho, yeye ni ndugu. Kwa sababu hapo ni mahali pamoja ambapo sote tunaweza kukutania. Ni njia ya Mungu ya kuifanya. Vitu hivi vingine ni kanuni za imani zilizobuniwa na wanadamu zilizoingizwa katika Hili. Lakini mpango asili wa Mungu kwa ajili ya msamaha ni chini ya Damu ya Yesu Kristo. Huo ndio mpango wa Mungu wa kuifanya. Naam.

108 Desturi katika siku hizo, nabii mashuhuri alipaza sauti, naye akasema, "Desturi zenu hazina nguvu. Zinanuka mbele Zangu. Sina imani nayo." Watu walikuwa wakitoa dhabihu hizi, pasipo hata kuwa na imani katika kile wanachofanya.

109 Sasa hebu tujiulize tu wenyewe swali hili. Hilo si ni jambo kama leo hii? Vibaya kadri tunavyochukia kulisema, inatubidi kukabiliana na kweli za mambo mahali fulani. Kuna kasoro mahali fulani.

110 Mbona, Kanisa hili linapaswa kuwa maili milioni moja huko barabarani, mbali na mahali lilipo sasa. Yesu anangojea Kanisa Lake kuwa tayari. "Bibi-arusi Wake amejiweka tayari." Tunao uwezo. Roho Mtakatifu yupo hapa. Mungu yupo hapa, nguvu za kuwaponya wagonjwa, nguvu za kufanya mambo yote ambayo Kristo alifanya. Nimeliona likidhihirishwa, mimi mwenyewe, na Roho Mtakatifu. Kwa hiyo, uwezekano upo hapa.

111 Kile Mungu anachotungojea sisi kuondokea, ni desturi zetu, na kurudi chini ya Damu ya Mwana Wake, Yesu Kristo, na kuwa Kanisa la Mungu aliye hai. Methodisti, Baptisti, Lutheri, Presbiteri, chochote zaidi, "Yeyote atakaye aweza kuja na kuchukua maji ya Uzima bure." Ninaamini hilo kwa yote yaliyoko ndani yangu. Sisi. . . Mungu ametuma chini Roho Mtakatifu kufanya hilo.

112 Lakini sisi, pamoja na desturi zetu za ibada, bila ya unyofu, sisi tukienda, ni kwa sababu ni—ni desturi yetu, na kwa sababu ni desturi ya ibada. Tunaenda bila unyofu, bila majuto halisi ya dhambi.

113 Nikitambua, hivi majuzi usiku, katika mkutano ule maarufu wa mmoja wa ndugu zetu mashuhuri anayejulikana huko California. Na nilitambua mkutano huo, watu hao waliposhuka, watoto wadogo matineja. Nilimpenda ndugu huyo kwa ajili ya msimamo wake mkuu; yeyote angempenda. Ukiweka mahali, uone ni mahali gani alipochukua katika siku za mwisho, utampenda pia. Na kama nilivyowaona wale watu wakishuka kuja madhabahuni, kufanya uamuzi, wasichana wakitafuna chingamu, wavulana wakipigana kofi, watu wakicheka, hiyo siyo njia ya kuja kwa toba ya kitauwa. Huna budi kuja chini ya ushawishi. Mungu, tutumie uamsho wa Roho Mtakatifu, wa mtindo wa kale, wa kipentekoste ambao utaleta dhambi kwenye mzizi na kushawishi wanaume na wanawake.

114 Si kusema, "Nitarudi kanisani na nitaufanya upya ushirika wangu. Nitatia sahihi kadi." Hiyo ni sawa, lakini unaweza kujiunga na Masoni, Jamaa wa Kipekee, na chochote kile, na upate matokeo yale yale.

115 Bali wakati unapokuja chini ya upatanisho wa Mungu unaosamehe wa Damu ya Yesu Kristo, hapana budi pawe na unyofu utakaoingia mle. Mungu anahitaji unyofu.

116 Kama ilimchukua gharama kubwa hivyo, kumtoa Mwana Wake wa pekee, tutapitaje, chini ya suala dogo la kucheka, na kuja kujiunga na kanisa, na kufanya uamuzi wa kadi na kuipeleka kanisani, na chochote kiwezacho kuwa? Hayo si matakwa ya Mungu. "Yeye apandaye katika machozi bila shaka atarudi tena, akishangilia, akileta pamoja naye mavuno ya thamani." Tunahitaji watu wanaoleta mavuno.

117 Nilimsikia mwinjilisti mashuhuri akisema, wakati mmoja nilipokuwa nikihudhuria moja ya viamshakinywa vyake,

akachukua Biblia...Na daima nilikuwa ninamtamani. Akasema, "Hiki hapa kigezo. Hicho ndicho Mungu anachohitaji." Akasema, "Nitaenda katika mji, nitakuwa na uamsho." Kasema, "Nitakuwa na elfu ishirini au thelathini watakaofanya uamuzi. Ninarudi katika yapata miaka minne au mitano, ama labda miaka miwili," na kasema, "Siwezi kupata kumi na watano au ishirini." Kasema, "Mtakatifu Paulo alienda katika jiji na akafanya mwongofu mmoja. Alirudi katika mwaka mwingine mmoja, alikuwa na thelathini au arobaini kutokana na huyo mmoja." Ndipo akasema, "Ni wahubiri wazembe ambao wanaketi huku miguu yao ikiwa juu ya dawati na hawatoki kuenda kuwaona watu."

118 Ninatamani ujasiri wake wa kuwakemea ndugu zake, na mambo juu ya msimamo wake. Bali ningependa kumwuliza swali hili, "Ni mhubiri yupi aliyemwambia yule mmoja huko nyuma chini ya Paulo, wakati hakuna makanisa kwake kuenda?"

119 Ilikuwa ni kitu gani? Paulo akimtoa katika desturi, au kutia sahihi kadi, kuingia katika ubatizo wa Roho Mtakatifu, wakati nafsi yake ilikuwa ikiwaka moto kwa ajili ya Mungu. Ilimbidi kushuhudia na kusema mambo. Nafsi yake yote ilikuwa ikiwaka kwa mwale wa moto ambao Mungu alikuwa ameweka humo. Tunachohitaji usiku wa leo ni ishara kwamba mwanaume au mwanamke ameokoka, waangalie wakizifuata nafsi zingine upesi wawezavyo.

120 Alisema wakati mmoja kwamba mhudumu wa baa... Mvulana mdogo aliingia na kusema, "Bw. Mhudumu wa Baa?"

Akasema, "Naam, mwanangu."

Akasema, "Ishara yako iko chini."

121 Akasema, "Vema, asante, mwanangu." Kwa hiyo akatoka nje, naye mvulana huyo mdogo akasimama huku ameweka mikono yake nyuma yake, naye mhudumu wa baa akatazama juu. Na kulikuwa na chumba kubwa cha baa kwenye kipande kikubwa cha shaba, kimetangazwa. Alichukua nguo yake na kuipangusa. Akasema, "Mwanangu, umekosea. Ishara yangu iko juu."

122 Akasema, "La, bwana." Kasema, "Haiko juu." Kasema, "Ninamaanisha ishara yako—yako bora zaidi."

Akasema, "Hiyo ndiyo ishara bora kuliko zote niliyo nayo."

123 Akasema, "Loo, la. Tazama, amelala *pale*." Pale alilala mlevi, kwenye mtaro. Hiyo ilikuwa ndiyo ishara bora kuliko zote aliyokuwa nayo, naam, bwana, wakati alipomwona mtu chini ya ushawishi wa kile alichokuwa akiuza ndani.

124 Na tunapomwona mtu chini ya ushawishi wa Roho Mtakatifu, mpaka maisha yake yanawaka kwa Moto wa pentekoste ya mtindo wa kale, hiyo ndiyo ishara iliyo bora kuliko zote Mungu aliwahi kuwa nayo kwamba mtu huyo

ameokoka, kama atatumika. Ndiyo ishara bora kuliko zote. Sasa, hiyo itakuja namna gani? Si kwa kujiunga na kanisa, bali kwa kukubali msamaha Wake kupitia Yesu Kristo, Kibadala chako kisicho na hatia.

125 Hakuna unyofu, hakuna majuto halisi kwa ajili ya dhambi. Alisema Yeye angeuficha uso Wake kutoka kwa desturi zao za ibada. Maombi yao hayakuwa na nguvu. Waliomba, loo, hakika. Walienda huko juu na kukariri sala zao. Walitoa sadaka zao. Ikawa desturi.

126 Je! wajua, katika Timotheo wa Pili, kifungu cha 3, ama mlango wa 3 wa Timotheo wa Pili, tunaambiwa jambo lile lile, kwamba tungepata katika siku za mwisho? Biblia ilisema hapa, "Katika siku za mwisho, fahamu hili, kwamba wakati utakuja ambapo watu watakuwa wakaidi, wenye kujivuna, wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu; wasiofanya suluhu, wasingiziaji, wasiotosheka, na wasiopenda walio wema; wakiwa na mfano wa utauwa, bali wakikana nguvu zake: hao nao mjiepushe nao. Kwa maana hawa ndio aina waendao nyumba hadi nyumba, na kuongoza wanawake wapumbavu, wakipotoshwa na tamaa mbalimbali, na daima—daima wanajifunza, na hata hawawezi kufikia ujuzi wa Kweli." Sasa, ikiwa Biblia imebashiri kwamba saa itafika ambapo kanisa litaingia katika desturi ile ile waliyokuwemo huko, kwa desturi zao za ibada, hii hapa tena, dini ya kimapokeo, isiyo na nguvu.

127 "Loo," walisema, "hao walikuwa wakomunisti." La, hawakuwa.

128 "Wakiwa na mfano wa utauwa." Wanaenda kanisani. Wanajiunga na kanisa. Wanajaribu kufanya o—onyesho refu, kwamba wanaenda kanisani na kadhalika, na kutoka na kuishi vinginevyo.

129 Hakuna moto moyoni mwao. Hakuna kitu. Hawavutiwi na yeyote mwingine. "Kila mtu mwingine anaweza kufa na kuenda wakitaka. Tunajisikia kwamba tumeokolewa. Acha hao wengine waende." Huo sio Ukristo halisi.

130 Ukristo ni: mfuate yule aliyepotea, nenda kamtafute ndugu huyo, nenda ufanye jambo kulihusu. Hivi tunaweza kusimama na kukunja mikono yetu, hata tukidai kwamba tumeokoka, na kuona wanaume na wanawake wakifa kila mahali? Na barabara, zimejaa wanawake wanaoenda makanisani, wakiwa na kaptura na—na nyuso zilizopakwa rangi, huku—huku wakitembea huku na huku mtaani, wakiwa na sigara mikononi mwao; na—na rangi usoni mwao mwote, inaonekana kama mbweha au mbwa mwitu, au kitu fulani. Na wanaume wakitembea huku na huku mtaani, wakijiunga na makanisa, na mambo kama hayo. Na kuita huo Ukristo, na kutulia?

131 Mtakatifu Paulo angefanya nini kama angetembea katika Tucson? Sasa, ninasema wangemtia gerezani kabla ya asubuhi. Hiyo ni kweli. Kwa nini? Nafsi yake ingewaka kwa ajili ya Mungu mpaka asingejizuia kufanya hilo. Hakika. Lakini tunajiunga na kanisa. Unaona, desturi zetu zimekuwa uvundo usoni pa Mungu.

132 Tunachohitaji leo hii ni nabii kuinuka jukwaani akiwa na "BWANA ASEMA HIVI" na kurarua vitu hivyo mpaka chini na kusema kwamba vimekuwa uvundo. Madhehebu yetu yamekua. Makanisa yetu ni makubwa, na ni mazuri kuliko yalivyowahi kuwa. Tungekuwa bora zaidi tukiwa na sufuria ya bati, tumesimama uchochoroni tena, tukiwa na gitaa, huko nje tukipiga ngoma, au kitu kingine, pamoja na Moto halisi wa kipentekoste ukiwaka nafsini mwetu, kuliko kuketi kwenye marefu mashuhuri tunayokalia leo hii, tukifa. Ulimwengu unakufa, chini ya miguu yetu. Naam, bwana.

133 Mungu anao msamaha, na msamaha huo ni kupitia Yesu Kristo pekee; elimu, desturi, dhehebu, sayansi, hakuna kitu kitakachochukua mahali pake. Ni chini ya hiyo Damu. Ni chini ya desturi . . . si desturi, bali chini ya Damu ya Yesu Kristo, njia ya Mungu iliyotolewa kwa ajili ya wenye dhambi, njia ya pekee tunayoweza kukutana.

134 Nakwambia, hebu chukua Mmethodisti, mchukue Mbaptisti, na Mpresbiteri, na Mlutheri, na Mpentekoste, na hebu kila mmoja aje chini ya hiyo Damu, hao ni ndugu. Hakuna kuzozana kuwahusu wakati huo. La, bwana. Hao ni ndugu. Wanaona kila kitu sawa. Lakini acha Mbaptisti aanze kuzozana na Mbaptisti, juu ya utaratibu wa ubatizo; acha wa Umoja azozane na wa Utatu, au Utatu na Umoja, na chochote zaidi, angalia mzozo na nywele zikisimama. Lakini hebu wote wawili waje chini ya msalaba, na uone kinachotukia.

[Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]
Na itakuwa hata nitakapokufa.

Ndipo katika wimbo mzuri, mtamu zaidi,
Nitaimba nguvu hizi za kuokoa,
Wakati maskini ulimi huu unaopiga kitembe,
na kugugumiza
Utakapolala kimya kaburini.

135 Ninatoa ushuhuda, usiku wa leo, kwamba Damu ya Yesu Kristo humfanya Mmethodisti, Mbaptisti, Mlutheri, Mpresbiteri, chochote alicho, ndugu yangu. Naam, bwana. Kuna kitu fulani katika jamaa, kwa sababu roho yake ni—ni ndugu. Yeye si mgomvi na—na kitu kingine. Ni . . . Yeye ni ndugu katika Kristo. Anaamini kila Neno lililoko katika Biblia hiyo.

136 Anawezaje Roho Mtakatifu, Yule aliyeandika Biblia, aikane? Anawezaje Roho Mtakatifu anayeishi ndani ya mtu, kusema, "Loo, hilo lilikuwa kwa ajili ya wanafunzi, ambao"?

Yesu alisema, "Yeyote atakaye."

137 Petro alisema, "Ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, wote walio mbali, hata wote ambao Bwana Mungu wetu atawaita." Roho Mtakatifu alikuwa kwa ajili ya yeyote yule Mungu alimwita.

138 Hapa Yeye alisema, "Wale ambao Yeye aliwachagua kimbele, Yeye aliwajua kimbele." Alichagua, nao wakakubali.

139 "Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu," alisema Yesu, "asipovutwa na Baba. Na wote ambao Baba amenipa Mimi watakuja Kwangu."

140 Je! tunakuja katika msisimko wa kuchochewa? Je! tunakuja kujiunga na kanisa? Je! tunakuja kwa sababu hatutaki kwenda kuzimu? Ama, je! tunakuja kwa sababu tunampenda Mungu, ambaye, "Alimtoa Mwana Wake wa pekee, ili yeyote amwaminiye Huyo awe na Uzima usio na mwisho"? Je! tunakuja kwa sababu ni sadaka ya upendo ambayo Mungu alitupatia, ili tuweze kuonyesha, kuonyesha hiyo?

141 Mungu anachukia dini isiyo na nguvu. Dini yao haina nguvu. Kwa hiyo inambidi Yeye kuifanya nini siku hii? Anachukia ninii. . . Kila wakati, katika Biblia, ambapo Mungu aliwahi. . . Nje, upande huu wa Biblia, kila mara kulipotokea marekebisho au uamsho, uliungwa mkono na ishara kuu na nguvu. Wakati Luther alipotokea, wakati Wesley alipotokea, wakati warekebishaji wote, Sankey, Finney, Knox, Calvin, yeyote, palipotokea, palikuwa na nguvu zilizodhihirishwa. Mahali alipo Mungu, Yeye ni wa kimbinguni. Ambapo Mungu anajidhihirisha Mwenyewe, hapana budi kuwa na vya kimbinguni.

142 Waangalie Mafarisayo katika siku ile waliokuja kwa Yesu, na wanazungumza kuhusu upole na wema. "Ni nani aliyekuwa mwema kuliko maskini kuhani? Ni nani aliyekuwa mashuhuri kuliko kuhani wao? Yeye huja kwako unapozaliwa. Kama kuna mzozo katika ujirani, yeye huja na kuutatua. Na yeye daima ni mpatanishi. Yeye ni mtu mwenye upendo. Unajua yuko hivyo. Wakati ukiwa kwenye shida, unaweza kwenda kwake, yeye anakusaidia. Vipi kuhusu mtu mwema?"

143 Halafu, kuzungumza kuhusu huyu Yesu wa Nazareti. "Huyu kuhani, tunajua baba yake alikuwa ni nani, baba ya baba yake, baba ya baba yake. Tuna shule hapa inayomtambulisha. Ni nani huyu Yesu wa Nazareti? Alitoka katika shule gani Yeye? Yeye ni mfuasi wa dhehebu gani? Yeye hufanya nini ila daima kuzozana? Anasema nini Yeye kuhusu huyo maskini kuhani wenu mpole? 'Yeye ni wa ibilisi,' Yesu alisema. 'Nyinyi ni—nyinyi ni. . . Ibilisi ndiye baba yenu, na kazi zake mtazifanya.' Unaweza kuwazia?"

144 Alienda huko juu hekaluni, akawatazama watu kwa hasira, akapiga teke kafara ambazo Yehova alihitaji, na kupaza sauti, "Imeandikwa, 'Nyumba ya Baba Yangu imefanywa nyumba ya maombi,' nanyi mmeigeuza kuwa pango la wezi."

145 Angefanya nini Yeye leo hii kama Yeye angekuja kwenye makanisa yetu ya kisasa? Kungekuwa na kusukumwa kwa meza tena, kungekuwa na kuruka marefu tena, kwa kuwa Yeye angelivuruga kwelikweli. Kweli. Ingekuwa ni jambo lile lile. Hivi hamwoni, Yesu ni wa Kimaandiko sana. Yeye alikuwa ni Neno. Haikumlazimu kuandika chochote. Yeye alikuwa ni Neno. Alikuwa ni Neno lililo hai. Nao watu wanakosa kulitambua.

146 Basi mtu anawezaje leo hii, juu ya kanuni za kile Yesu alichoahidi: ishara hizi ulimwenguni kote; na baraka hii kwa ulimwengu wote; na Roho Mtakatifu kushuka sawa tu na alivyofanya mwanzoni, juu ya yeyote ambaye Mungu angemwita; mtu anawezaje kujiita mwenyewe Mkristo, na kulikana hilo Neno, na kusema kwamba Roho Mtakatifu yuko ndani yake? Roho Mtakatifu ataitikia kila Neno la Mungu kwa "amina." Hiyo ni kweli kabisa.

147 Loo, ndugu, mifumo yetu ya elimu imetupeleka mbali nalo. Nayo ma—madhehebu yetu yametutenganisha mmoja na mwenzake na kutoka kwa Kristo. Lakini, kitu gani? Wataendelea kufanya hivyo. Na wewe ukichukua kibadala, kitu kingine chochote, si zaidi ya majani ya mtini tena. Mungu anakikataa. Bali Kanisa likija chini ya Damu ya Yesu Kristo, wakiwa na ishara ya Roho Mtakatifu juu yao, basi unaenda kuona udugu tena. Unaenda kuona Kanisa lililojaa nguvu. Unaenda kuona.

148 Mungu anachukia dini isiyo na nguvu. Lazima iwe nguvu. Hakika. Ni nguvu za kuokoa mtu kutokana na dhambi. Ni nguvu zinazoweza kufanya ishara na maajabu na miujiza kama Yesu Kristo alivyoahidi. Walielekeza mawazo yao kwenye Neno la Mungu huko nyuma na kuliamini, na kugonga shabaha. Wewe elekeza mawazo yako vivyo hivyo kwenye Neno la Mungu; itagonga shabaha tena. Inabidi igonge, kwa sababu Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele. Mungu hapendi dini isiyo na nguvu. Mungu hataki hiyo. Mungu anataka kufanya kazi. Mungu anataka kujionyesha Mwenyewe akiwa hai. Matumaini yetu yenyewe ni ufufuo. Je! hiyo ni kweli? Matumaini yetu ya uzima ni ufufuo, ufufuo wa Yesu Kristo.

149 Mnaona, Mungu anataka kufanya kazi katika kanisa Lake. Yesu alisema, "Nitakuwa pamoja nanyi daima, hadi mwisho wa ulimwengu. Kazi nizifanyazo nanyi mtazifanya pia." Yohana Mtakatifu 12:14, "Kazi nizifanyazo nanyi mtazifanya pia; hata zaidi ya hizi mtafanya, kwa kuwa ninaenda kwa Baba Yangu." Sasa, kanisa hujaribu kukana hilo, kuenda—kuenda kutafuta washiriki zaidi, kuwa maarufu zaidi.

150 Sasa ninataka kuwaulizeni jambo fulani. Mungu anajaribu kufanya kazi katika kanisa Lake, nalo kanisa linajaribu kufanya kazi kwa kanuni ya imani, na hizo mbili haziwezi kufanya kazi pamoja. Inakubidi kuondoa kanuni ya imani, na kumfanya Kristo aingie. Basi unawezaje kufanya hilo? Wakati Yeye akiona

Damu, wakati Damu imewekwa pamoja na moyo mwaminifu, na mkono kuwekwa juu ya Yesu Kristo, na moyo ulio wa kweli mbele za Mungu; kukiri makosa yake na kuzaliwa na Roho Mtakatifu, ndipo kazi za Mungu zitafuata, kama Yeye alivyosema zitafanya. Naam, kanisa linataka kufanya kazi kupitia kanuni zao za imani, na kuona ni wafuasi wangapi wanaoweza kupata. Mungu anataka kufanya kazi kupitia nguvu za Damu, kuwafanya Wakristo wazaliwe upya. Hiyo hasa ndiyo tofauti yake.

151 Kufanya, lazima, huna budi kukataa. Kufanya hili, wao, inakubidi kumkataa Roho Mtakatifu na nguvu Zake za utendaji, kukubali kanuni ya imani. Inakubidi kuiona Kweli kabla ya kuweza kukubali uwongo, kama unaenda kuwa Mkristo. Huwezi. . .Inakubidi kuikanyaga ahadi ya Mungu, ili uweze kuchukua uwongo. Kwa sababu, ipo taa nyekundu inayomulika mbele zako, wakati wote, "*Hili* ndilo Neno."

152 Unasema, "Vema hiyo ilikuwa ni kwa ajili ya siku nyingine." Ni kwa ajili ya leo hii, kwa sababu Kristo ni Neno. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Yohana Mtakatifu 1, "Hapo mwanzo alikuwako Neno, naye Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili akakaa katikati yetu." Nayo Biblia ilisema, "Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele." Kwa hiyo, kama Kristo ni Neno, kila ahadi ni kweli, na ni lile lile jana, leo, na hata milele. Inabidi liwe. Inahitaji imani iliyozaliwa tena kuliamini na kuliingiza kazini. Ninii, huwezi kulifanya na desturi. Halitafanya kazi. Inakubidi kuja kwenye Damu hiyo, kwa hakika tu kama chochote. Baada ya Israeli kuambia . . .

153 Baada ya Isaya kuambia Israeli kwamba walikuwa wamechafua kibadala chao kwa desturi zao, kulitokea nabii mwingine. (Kabla hatujafunga.) Nabii mwingine mashuhuri akaja jukwaani, na huyo alikuwa ni Yohana mbatizaji. Sasa, aliwaelekeza kwa Mwana-kondoo ambaye angechukua. . . angefanya si tu kwa Israeli, bali wote wa jamii ya Adamu iliyoanguka. Alisema kulikuwa na. . .Mungu alikuwa anaenda kumtuma Mwana-kondoo. Na huyu Mwana-kondoo atakuwa ni kwa ajili ya Mmataifa, Myahudi, na yeyote atakayekuja.

154 Haikuwa muda mrefu sana mpaka huyo Mwana-kondoo alipotundikwa kwenye msalaba wa madhabahu Yake. Damu Yake ilimwagika. Roho Mtakatifu akarudi. Sasa, wakati mwana-kondoo mnyama wa kale alipokufa, roho wa mnyama asingeweza kurudi, kwa hiyo damu hiyo iliwekwa tu kwa taifa. Lakini sasa, kwa ajili ya jamii yote ya Adamu, Mwana-kondoo wa Mungu aliyemwagwa, Damu Yake, ishara ilirudi katika umbo la Roho Mtakatifu, kuja juu ya mwabuduo. Sasa, hilo ndilo Mungu analohitaji. Hilo ndilo walilofanya katika siku ile. Na hilo ndilo wata. . .wanafanya leo hii.

155 Sasa, kama watu wowote wanahisi uzito wa dhambi, na unajua kwamba uko makosani, sikiza, kuna msamaha, na msamaha huo ni kupitia Mwana-kondoo wa Mungu. Mnaamini hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Ni kupitia Mwana-kondoo, kupitia Damu ya Mwana-kondoo.

156 Nilisimuliwa hadithi ndogo wakati mmoja. Ilinisaidia sana. Kulikuwa na mvulana aliyetekwa nyara katika siku za mwanzoni. Nadhani nyinyi nyote mmesoma historia ya Biblia na kusoma historia ya kanisa. Na katika . . . Naamini kilikuwa cha Foxe . . . La, hakikuwa. Kilikuwa ni Baba wa Nikea, ama maisha ya Mtakatifu Patrick. Mtakatifu Patrick alikuwa hasa . . . Hilo lilikuwa tu ni jina alilopewa. Jina lake lilikuwa Succat. Naye alikuwa—alitekwa nyara na kundi la—la maharamia wa baharini na akakodiwa, kuwa mlishaji nguruwe.

157 Na hadithi hii inaenda kwamba mtoto huyu alitekwa nyara na kupandishwa kwenye meli, na alikuwa anatafuta njia yake. Ndipo maskini nahodha akawa mgonjwa siku moja na alikuwa—alikuwa karibu tu kufa. Naye alikuwa mgonjwa sana, huko mbali baharini, na maskini jamaa huyo mwenye ndevu zilizoingia mvi, akilala katika kijumba chake. Ndipo akaita wasaidizi wake, watu wake wa sitaha, kasema, "Hivi kuna Biblia miongoni mwenu?" Kasema, "Nilipokuwa m—mtoto, nililelewa Kikristo." Tena kasema, "Mimi, ninakufa. Na—na, jamani, sitaki kufa namna hii." Akasema, "Hivi mna Neno la Mungu? Mtu yeyote hapa ana Neno la Mungu?"

158 Hatimaye, huko nyuma kwenye kundi la wanaume, mvulana mdogo alisimama, naye akasema, "Bwana, ninayo Biblia. Mimi ni Mkristo. Mimi huibeba pamoja nami."

159 Akasema, "Njoo hapa, mwanangu." Akasema, "Unamaanisha wewe hubeba Biblia?"

160 Akasema, "Naam." Kasema, "Mama yangu na baba walikuwa Wakristo, na mimi nikatoa maisha yangu kwa Kristo wakati nilipokuwa tu ni jamaa mdogo, na mimi nimelibeba Neno Lake pamoja nami popote niendapo." Kasema, "Nililiweka Hilo moyoni mwangu na Hilo limekuwa moyoni mwangu."

161 Akasema, "Nisomee kitu kutoka hapo, mwanangu, kabla sijafa."

162 Ndipo jamaa huyo mdogo akageukia Isaya 53:5, "Nalo linasoma hivi, 'Alijeruhiwa kwa makosa yetu. Alichubuliwa kwa uovu wetu. Adhabu ya amani yetu ilikuwa juu Yake. Na kwa mapigo Yake sisi tumepona.'"

163 Basi aliposema hivyo, maskini nahodha huyo akasema, "Unaweza kusoma ukiendelea?"

Maskini mvulana huyo akasema, "Naweza kutoa tamshi hapa?"

Naye maskini nahodha akamwambia mvulana huyo, kasema, "Endelea."

164 Akasema, "Mama yangu Mkristo, kabla sijaondolewa kwake, kasema . . . Unajua, yeye alizoea kunisomea Andiko hilo, sana. Na unajua jinsi ambavyo yeye alilisoma?"

165 Naye maskini nahodha akasema, "La, mwanangu. Ningependa kusikia jinsi mama yako Mkristo alivyolisoma."

166 "Akasema . . . " Akasema, "Hivi hapa jinsi alivyolisoma, 'Alijeruhiwa kwa makosa ya Willie Pruitt. Alichubuliwa kwa uovu wa Willie Pruitt. Adhabu ya Willie Pruitt ilikuwa juu Yake. Na kwa mapigo Yake Willie Pruitt alipona.'"

167 Maskini nahodha huyo akasema, "Ninapenda hilo. Ninapenda hilo." Kasema, "Loo, laiti jina langu lingaliweza kusomwa humo ndani!" Kasema, "Unafikiri ungeweza kulisoma, mwanangu?"

168 Akasema, "Nitajaribu." Akasema, "Alijeruhiwa kwa makosa ya John Quartz. Alichubuliwa kwa uovu wa John Quartz. Adhabu ya amani ya John Quartz ilikuwa juu Yake. Na kwa mapigo Yake John Quartz alipona."

169 Huku machozi yakitiririka chini ndevuni mwake, alisema, "Nileteeni nguo zangu. Yesu Kristo ameniponya. Ninatoa maisha yangu Kwake." Unaona?

170 Loo, rafiki, laiti ungaliweza tu kusoma jina lako humo ndani! Loo, kama ninaweza kusoma jina langu, "Alijeruhiwa kwa ajili ya makosa ya William Branham. Alichubuliwa." Si kanisa, si ninii tu . . . si kanuni ya imani. "Bali Yeye alichubuliwa kwa uovu wangu. Adhabu ya amani yangu ilikuwa juu Yake. Na kwa mapigo Yake William Branham alipona." Loo, laiti tungaliweza tu kusoma jina letu katika Maandiko, na kwa kweli tumaanishe, ni hilo ndilo hufanya kazi. Kusoma jina letu ndani yake, huleta kupokea, msamaha, kwa kuwa tukitambua kwamba Yeye alijeruhiwa kwa makosa yetu, Yeye alichubuliwa kwa uovu wetu.

171 Kitu kingine, tunaona katika Waebrania 9:11, kwamba msamaha huleta usafi, mwabuduo kuwa bila ya dhamira ya dhambi tena, na amejitakasa mwenyewe kutokana na desturi zilizokufa. Wakati kweli tumekuja chini ya Damu, tunatakaswa kutokana na mapokeo yaliyokufa. Maandiko yanasema hivyo, Waebrania 9, angalia, "Itawasafisha dhamiri zenu kutokana na mapokeo mafu." Basi, ukifanya hivyo, sahau kwamba wewe ni Mbaptisti, sahau wewe ni Mmethodisti, sahau wewe ni Mpentekoste, chochote ulicho, na uyasahau hayo mapokeo mafu, na uje kwenye Damu. Njoo kwenye hiyo.

172 Lisome jina lako katika hiyo, halafu ufanye hili, ndipo uje kwenye meza ya ushirika, ndipo uje na uone ni nani aliye sahihi na asiye sahihi, kama utakuwa ushirika uliotengwa au la, uone

ikiwa unaweza kumfungia ndugu yako nje. Huwezi kufanya hivyo. Huwezi kabisa kufanya hivyo. Kuna kitu ndani yako, hakitakuruhusu kufanya hivyo. Kuna kitu tu, unaona. Jina lako linasomwa miongoni mwa wale na huwezi kufanya hivyo. Hiyo hukutakasa. Hiyo hukusafisha.

173 Kumkumbuka Yeye wakati tunapopiga magoti kwenye msalaba, acha awe kasisi wa Katoliki, Presbiteri, chochote awezacho kuwa. Acha mtu huyo aje jinsi anavyosoma jina lake mle ndani, "Alijeruhiwa kwa makosa ya kasisi *huyu*. Alijeruhiwa kwa ajili ya huyu Mmethodisti, huyu Mbaptisti, huyu Mpentekoste." Kitu gani? "Alijeruhiwa kwa makosa yetu," jina langu, jina lako, chochote ulicho. Basi hebu tuamini Hilo; si kile kanuni ya imani isemacho. Kile Neno lisemacho! Halafu acha tupige magoti kwenye msalaba, pamoja. Sisi ni ndugu. Loo, naam, mapokeo, tunajitakasa basi kutokana na mapokeo yote mafu.

174 Kungeweza kuwa na wazee wa jimbo arobaini, kungeweza kuwa na makuhani wakuu arobaini, kungeweza kuwa na makadinali, na maaskofu, na mapapa, kila kitu kingine, wakipiga mayowe, "Amka kutoka hapo. Usijichafue." Lakini wewe umemkumbatia ndugu yako, ndugu. Kuna kitu halisi. Umepata msamaha chini ya Upatanisho ule ule ambao kwao yeye amesamehewa. Nyinyi ni ndugu, na inanata karibu zaidi ya ndugu. Ni kitu fulani kukihusu, ambacho hukuvuta karibu sana na Mungu. Na wakati mnaposonga karibu na Mungu, mnasonga karibu mmoja na mwenzake.

175 "Unawezaje kumchukia ndugu yako ambaye unamwona, ama kumdharau, na kusema unampenda Mungu Yule ambaye hujamwona? Unakuwa mwongo, nayo Kweli haimo ndani yako."

176 Bali tukifikia mahali, ambapo Damu ya Yesu Kristo hutusafisha kutokana na dhambi zote, basi sisi ni ndugu. Basi hakuna tofauti ndani yetu. Maskini vibandiko vyetu vya kale ambavyo vimebandikwa juu yetu, havimaanishi chochote.

177 Ninakumbuka pale, nilipita lango hivi majuzi na nilikuwa nikimwonyesha mmoja wa ndugu aliyeketi hapa, ambapo nilizoea kulisha ng'ombe. Na nikija kupitia hapo, mhifadhi angeangalia ng'ombe hao walipokuwa wanapitia katika mkusanyiko wa kuchipua. Na yeye aliangalia. Kamwe hakuninii . . . Walikuwa na kila namna ya chapa juu yao. Lakini yeye kamwe hakuangalia chapa. Aliangalia kibandiko cha damu. Na ilibidi awe ni Herefodi ukoo safi la sivyo asingeweza kuenda kwenye Msitu wa Arapaho, kwani Shirika la Herefodi lililishia pale. Ilibidi awe ni Herefodi ukoo safi.

178 Nafikiri hivyo ndivyo itakavyokuwa kwenye wakati wa mwisho. Yeye hatasema, "Je! wewe ni Mmethodisti? Je! ulikuwa Mbaptisti?"

179 Hilo ndilo swali kubwa leo hii, "Nini—wewe ni kitu gani? Je! wewe ni Mmethodisti, Mbaptisti?"

Nikasema, "La."

180 "Wewe ni kitu gani; Presbiteri, Lutheri, Nazarayo, Pentekoste?"

"La."

"Wewe ni nini?"

"Mkristo."

181 Mkristo, kibandiko cha Damu, unaona, chini ya Damu. Hiyo inamaanisha kwamba kila ndugu, dada chini ya Damu hiyo ni ndugu yangu, dada. Unyofu wa kilindi mno hapo mbele za Kristo. Sisi, kasisi, mhubiri, chochote zaidi, tuweke mikono yetu juu ya dhabihu yetu na kusema, "Sisi ni wenye dhambi walio na hatia. Hatustahili rehema Zako, Ee Mungu. Bali Wewe ulimtuma Mwana Wako kufa mahali petu, nasi tunaipokea kwa njia huru." Loo, sisi ni ndugu basi.

182 Mizozo yote ya kale imeisha. Yote imetoweka. Kwa kweli tumesamehewa. Wewe nenda, umesamehewa na kutakaswa kutokana na dhambi, umetakaswa kutokana na mapokeo. Vitu vya kale vimepita. Mizozo ya kale imeisha. Wabaptisti wote, Methodisti, na Presbiteri wote wametakaswa kwa Damu ile ile, na sisi tunakuwa ndugu. Mizozo ya mapokeo imeisha, basi tunaweza kushiriki pamoja. Na hapo, pekee, tunaweza kushiriki.

183 Nimewaona Wapresbiteri wakisimama katika mikutano hii ya Wafanyabiashara wa Full Gospel, wakinena kwa lugha na kupaza sauti kwa nguvu walivyoweza, na baadhi ya Wapresbiteri maarufu kuliko wote walioko Marekani. Jim Brown, ni wangapi waliwahi kukutana na yeye, Mpresbiteri maarufu, akisimama hapa na kucheza katika Roho, na kunena katika lugha, na kuendelea hapa, na mchungaji wa moja ya Makanisa maarufu sana ya Presbiteri katika Marekani. Walutheri, Wamethodisti, Pres-. . . wote pamoja, ni kitu gani? Wamekuja chini ya Damu. Hakuna vibandiko. Hakuna vizuizi vya kidhehebu. Sisi ni kitu kimoja. Sisi ni Wakristo. Tuna vitu shirika. Naam. Hapa muda si mrefu uliopita . . .

184 Katika kufunga. Kulikuwa na mwanaume na mwanamke, mume na mke, walikuwa wanatengana. Na walijaribu kupatana. Walienda kwa wataalamu wa magonjwa ya akili, kuona ikiwa angeweza kuleta nia zao pamoja, bali asingeweza. Walienda kwa kila kitu ambacho wangeweza kufikiria, kujaribu kuishi pamoja, lakini waligombana tu, na siku zote walitengana. Na kabisa wasingeweza kuvumiliana, na wasingeweza kusimama uweponi mwa kila mmoja, na wanaanza kuzozana. Kwa hiyo, waliamua wangetalikiana.

185 Kwa hiyo, walikodi mwanasheria, kuwapa talaka. Naye akasema, "Vema, sasa, kabla hatujafanya hivyo," kasema,

"tunapauza mahali hapo." Tena kasema, "Nyote afadhali mwende huko na mgawe mali kati yenu kabla hamjapata talaka na mahali hapo kuuzwa."

186 Kwa hiyo, mume na mke wakaenda pamoja. Wakaenda kwenye nyumba. Basi wakaingia sebuleni, naye mke akasema, "Ninaenda kuchukua *hiki*."

Na mume akasema, "Ninaenda kuchukua *hiki*."

187 Ndipo wakazozana, na wakagombana na kufanya yasiyofaa, mmoja na mwenzake. Baada ya kitambo, wangesema, "Vema, nitakupa *hiki* kama utachukua *hiki*." Vema, hilo liliendelea kwa kitambo. Ndipo wakaenda sebuleni na mahali mbalimbali, na kuingia jikoni, na kuingia chumba cha kulala. Waligawana mali yao.

188 Ndipo hatimaye wakakumbuka kulikuwa na vitu fulani kwenye dari. Kwa hiyo walipanda juu kwenye dari na kuvuta kasha la kale. Ndipo wakaanza kutoa vitu mbalimbali, kasema, "Unaweza kuchukua *hiki*, na unaweza kuchukua *hiki*." Na hatimaye macho yao wote wawili yakaangukia kitu fulani kidogo, na wote wawili wakakinyakua. Ndipo wakatazamana. Kilikuwa ni kitu gani? Jozi ya vijiatu vidogo vyeupe ambavyo vilikuwa vya mtoto mchanga ambaye alikuwa amefariki. Kilikuwa ni sehemu yao wote wawili. Hapo, huku mikono yao ikiwa imeshikana namna hiyo, juu ya viatu vya mtoto huyu mchanga. Kwa kweli, kilikuwa ni cha nani? Kilikuwa cha nani? Kilikuwa chao wote wawili. Walikuwa na vitu shirika.

189 Katika dakika chache, wakati mmoja akimtazama mwenzake, machozi yakaanza kutiririka chini mashavuni mwao. Kilikuwa ni kitu gani? Wangeweza kugawa kila kitu, lakini wakati walipokuja mpaka walipokuwa na kitu fulani shirika, mtoto, naye alikuwa mbinguni, ndipo mzozo ukaisha. Katika dakika chache, walikuwa wamekumbatiana. Talaka ilitatuliwa. Amani ikatawala.

190 Basi, ndugu, hebu niwaambieni hili usiku wa leo. Hatuwataki mjiunge na kanisa. Lakini ninawaulizeni hili. Lipo jambo moja tulilo nalo shirika, hilo ni Yesu Kristo. Yeye yuko shirika pamoja nasi. Sisi sote hatuwezi kuwa Wabaptisti. Hatuwezi sote kuwa Methodisti. Sote hatuwezi kuwa Umoja, au Utatu, ama chochote kile. Hatuwezi kuwa hicho. Lakini kuna jambo moja tulilo nalo shirika, hilo ni toleo la msamaha wa Mungu, Mwana Wake, Yesu Kristo. Tuko na vitu vyote ndani Yake. Lakini hicho ndicho kitu cha kwanza kwetu kukubali. Ndipo tunaweza kupata vitu vingine, tunapokubali msamaha ambao Mungu ametupatia. Na hiyo haitakuwa kupitia mfumo wetu wa elimu, kupitia mfumo wetu wa kidhehebu, bali itakuwa kupitia Damu ya Yesu Kristo. Sisi sote tunaweza kukutana hapo chini ya msalaba, na kuwa kitu kimoja na kuwa na vitu shirika.

Mnaamini hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Hebu tuinamishe vichwa vyetu kwa muda mfupi tu tunapoomba.

[Dada mmoja anaanza kuhimiza. Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Amina.

191 Huku vichwa vimeinamishwa, hakika mioyo imeinamishwa, hebu tuinamishe mioyo yetu kwa dakika moja sasa, pamoja na vichwa vyetu, ukisema, "Bwana, huku nimeinamisha moyo wangu sasa, pamoja na hayo yote ya desturi yangu, je! niko sahihi ama makosani?" Jalia Roho Mtakatifu achunguze kupitia moyoni sasa. Na ikiwa si tu mahali inapaswa kuwa, na ungependa kukumbukwa katika maombi katika kufunga, hata unajua kwamba sote tunaweza kukutana chini ya kitu kimoja, Damu, Upatanisho. Ndipo tukifanya hivyo, basi tunatakaswa kutokana na vitu vyote vya ulimwengu. Na ungependa kukumbukwa katika maombi, waweza kufanya ijulikane kwa kuinua mkono wako kwa Mungu? Useme, "Ku-. . . " Mungu akubariki. Loo, jamani, mikono hiyo! "Nikumbuke, Ee Bwana."

192 Hivi unatambua kwamba hatuna siku zingine nyingi kuzunguka kupitia dunia hii? Unasema, "Vema, mimi ni kijana." Ninajua. Sijui, dada, ndugu, kutakuwa na matineja wengi watakaokufa usiku wa leo, kote ulimwenguni, mamia ya hao. La, kitu pekee ulicho nacho ni pumzi hilo lililobaki ndani yako.

193 Je! wewe, kwenye wakati huu, utasema, "Huku nimeinua mkono wangu, Bwana Mungu, ninakubali msamaha ambao Wewe umetoa, Damu ya Yesu Kristo; sasa jalia Ishara iliyotoka kwenye Damu, Roho Mtakatifu, aje juu yangu; sijampokea Roho Mtakatifu; ni—ninajua hilo; pia ni—ninataka kupokea hicho *Kitu fulani* ambacho hunifanya kujisikia vivyo hivyo unavyozungumzia, kwamba dhambi zangu zote zimeondolewa, na ulimwengu, upendo wa ulimwengu, umeondoka kwangu, na mimi ni kiumbe kipya; ninataka kujua hilo moyoni mwangu; pia, Mungu, simwinulii mkono wangu Ndugu Branham, bali ninakuinulia Wewe; na Wewe unaujua moyo wangu"? Na mtu yeyote asiangalie juu. Acha tu Mungu aone huu, peke yake. Na useme, "Mungu, ni—ni—ninataka Ishara, kwamba Damu imewekwa kwangu. Na mimi ninaitaka."

Inua mkono wako, useme, "Niombee, Ndugu Branham." Bwana akubariki. Hilo ni jema.

194 Haijalishi wewe ni kitu gani, Methodisti, Baptisti, Presbiteri, ni kwa ajili ya yeyote atakaye. Sasa, nina. . .sisemi chochote dhidi ya hayo makanisa. Wao, wako sawa. Lakini kile ninachojaribu kusema, kwamba hilo halitaokoa. Unaona?

195 Hauna budi kuwa ni msamaha wa Mungu, neema inayosamehe. Nayo imewakilishwa tu, si kupitia kanisa, bali kupitia Damu ya Yesu Kristo. Huyo ndiye Kibadala chako, wakati unapoweza kuweka mikono yako juu Yake na kusema, "Sasa ninakikubali kibadala hiki. Mungu, nirehemu."

196 Tena labda huenda kuna washiriki wa kanisa hapa, ambao wamejiunga na kanisa, kwa unyofu wote wa moyo. Ninaamini hilo, kwa moyo wangu wote, ulijiunga kwa unyofu. Lakini, unasema, "Ndugu Branham, kwa kweli, moyo wangu haujatakaswa kutokana na mapokeo haya yote na kadhalika. Ni—ninaamini kama mtu angenena dhidi ya kanisa lile hasa ambalo mimi...Kama Biblia hata ingesema, iniambie, ningethibitishwa na Biblia kwamba kanisa langu liko makosani, bado ni—nisingekubali hilo kutoka moyoni mwangu. Nisingekubali, bali ninataka kukubali. Niombee." Waweza kuinua mkono wako, useme, "Omba?" "Nitafanya hivyo. Naam, hakika nitafanya." Mungu akubariki. Hilo ni jema. Hilo ni sawa. "Ni—ninataka kuweza kukubali kila kitu ambacho Mungu alisema, vile tu Yeye alivyosema katika Biblia Yake. Pia ninataka Damu ya Yesu Kristo ije juu yangu."

197 Na Damu ikiwekwa, ishara! Unaona, ipo ishara inayotolewa ya Damu, na hiyo ni Roho Mtakatifu. Basi wakati Roho Mtakatifu aliposhuka, kwenye Siku ya Pentekoste, mnajua kile Huyo aliwafanyia watu. Na kila wakati Huyo atakapowahi kuja juu ya watu, Huyo atafanya jambo lile lile. Petro alisema, "Kwa kuwa ahadi ni kwa ajili yenu, kwa watoto wenu, kwao walio mbali, hata wote ambao Bwana Mungu wetu atawaita," ahadi hii hii.

198 Kama senti kumi ni senti kumi *hapa*, ni senti kumi *kule* nje. Ni, popote ilipo, ni senti kumi. Kama hii ni almasi *hapa* ndani, ni almasi *mle* ndani. Kama hii ni nyumba *hapa*, ni nyumba *kule*.

199 Na kama huyu ni Roho Mtakatifu aliyeshuka kwenye Siku ya Pentekoste, ni Roho Mtakatifu yule yule leo hii. Na wewe hujawahi kupata tukio hilo? Likubali sasa tunapoomba, sivyo?

200 Baba yetu wa Mbinguni, tukijua kwamba—kwamba jua linateremka upesi, wakati hautakuwepo tena, siku moja Malaika mkuu atajitokeza kwenye jukwaa la wakati, kutoka katika Umilele. Na parapanda ya Mungu italia, ndipo kila mwanaume na mwanamke watajibia kile ambacho tunakijua kuwa Kweli, Neno la Mungu. Hapana budi kuwepo na kigezo fulani ambacho inabidi Mungu awe nacho hapa duniani, ambacho tutahukumiwa kwacho. Na kama tungechukua kigezo cha kanisa letu, dhehebu letu, jinsi tungelikosa kwa mbali! Basi ni dhehebu gani lingekuwa sahihi? Hivyo basi, tungechanganyikiwa. Tusingalijua jambo la kufanya. Bali kuna kigezo, na hicho ni Neno Lako.

201 Nalo Neno Lako lilisema, "Mtu asipozaliwa mara ya pili, hawezi hata kuona Ufalme wa Mungu." Kwa maneno mengine, hawezi kuuelewa. Hana budi kuukubali kwa imani, na azaliwe tena, ndipo basi atauelewa. *Kuona* ni "kuelewa."

202 Basi tunaomba, Mungu, usiku wa leo, kwamba mingi ya mikono hiyo inayoinuliwa usiku wa leo, kote jengoni,

wafanyabiashara wa jijini, na wanawake, wavulana, na wasichana, ninaamini kwa unyofu wanainua mkono wao. Sasa, wasingeweza kuinua mikono yao isipokuwa kulikuwa na imani. Basi Roho Mtakatifu, kupitia wao, amewathibitishia kwamba wako makosani, na kuleta imani kwamba wanataka kuwa sahihi. Nao waliinua mikono yao Kwako, Muumba mkuu, wakijua kwamba inawabidi kukutana na Wewe siku moja. Nao walikuwa wanyofu, ninaamini, Bwana, nami ninaombea kila mmoja wao. Ninatumaini, usiku wa leo, Bwana, ninapoomba, kwamba hakuna hata mkono mmoja ulioinuliwa utakaoweza kuwa na utulivu mpaka Roho Mtakatifu ameyajaza maisha yao. Tujalie, Bwana. Ninawadai kwa ajili ya kumbukumbu za ushindi wa Yesu Kristo. Litimize, Bwana, ninaomba. Waokoe waliopotea.

203 Wajaze wale waliompokea Kristo, na Roho Mtakatifu. Mimina Huyo juu ya nafsi zao, Baba. Jitwalie Mwenyewe utukufu.

204 Yesu, Wewe umetwambia, "Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu asipovutwa na Baba Yangu kwanza," na, "Imani huja kwa kusikia, na kusikia Neno la Mungu." Basi sasa, Neno la Mungu linapohubiriwa, imani huja kwa kusikia. Nao wamevutwa, kwa sababu Biblia ilisema, "Wale ambao Yeye aliwajua tangu asili, Yeye aliwakusudia kimbele. Na wale ambao Yeye aliwakusudia kimbele, Yeye aliwaita. Na wale ambao Yeye aliwaita, Yeye aliwapa Uzima wa Milele."

205 Basi sasa, nyuma katika mwanzo, kabla ya ulimwengu, Wewe uliweka majina yao juu ya Kitabu cha Uzima cha Mwanakondoo. Na usiku wa leo Roho Mtakatifu amewaita. Nao wakainua mikono yao. Sasa, Bwana, wape Uzima wa Milele. Ninaomba hayo kwa ajili ya utukufu wa Mungu, kwamba Roho Mtakatifu atashuka ndani ya mioyo yao na kuwatahiri kutokana na kazi zote zilizokufa na mapokeo, na kuwapa msamaha bure. Na kuwajaza na Uwepo Wake, kwamba waweze kuenenda kuanzia siku hii, katika saa ya giza, kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma ambapo wanawake waliojipaka rangi usoni, utovu wa maadili ulitikisa mataifa.

206 Ee Bwana Mungu, naomba wanaume na wanawake waenende kama mioto inayowaka. Jalia Roho Mtakatifu kwa njia halisi atume Moto mtakatifu juu yao, Bwana, mpaka watajaa sana na wema wa Mungu, na—na kwamba wao wataenenda, kumwita kila mwenye dhambi wanayekutana naye, kwenye msalaba. Tujalie, Bwana, ambapo wao pia wanaweza kuanguka na kupata msamaha. Wafanyie hilo Methodisti, Baptisti, Presbiteri, Wapentekoste, na wote, Bwana. Tujalie. Hao ni Wako sasa. Ninawakabidhi mikononi Mwako, kwamba Wewe utawajalia hili. Katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

207 Mnampenda? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Na . . . Hili kidogo huenda likawa nje ya utaratibu. Kidogo tu. Hebu tuimbe wimbo huu mzuri wa kale wa kanisa. Ni—ninapenda kuimba. Mnajua, ninii . . . Wakati mwingine, katika kuhubiri, unasema mambo ambayo yanakata, bali kuna—kuna zeri katika Gileadi, sivyo, ambayo huponya nafsi? ["Amina."]

208 Hebu tuimbe wimbo huu mzuri, wa kale, kama mtaweza. "Nampenda, nampenda kwani alinipenda kwanza." Je! mnaujua wimbo huo? ["Amina."] Mtu fulani sasa aniongozee huo.

Nampenda, nampenda
Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

209 Hebu tuuvumishe. [Ndugu Branham anaanza kuvumisha *Nampenda*—Mh.] Sasa, wakati mnavumisha *Nampenda*. Ni Wabaptisti wangapi wapo hapa? Inua mkono wako. Wapresbiteri, Lutheri, Nazarayo, Pilgrim Holiness, Wapentekoste? Hapo, jamani, kwenye watu! Sote pamoja . . . [Ndugu Branham anaendelea kuvumisha *Nampenda*.] Tumefanya nini sasa wakati tumekuja chini ya msalaba, chini ya neema inayosamehe? Sote tumesamehewa, si na kanisa letu, bali kwa Kalvari.

210 Hebu tupeane tu mikono na Methodisti, Baptisti, na Pentekoste, sasa, tunapoimba tena. "Na . . . " [Ndugu Branham anapeana mikono na wale walio karibu na yeye—Mh.]

Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Kalvari . . .

211 Sasa, tunauimba ili kila mmoja aweze kuusikia. Sasa hebu tuinamishe tu vichwa vyetu na kuinua mikono yetu yote miwili kwa Mungu. Na kwa moyo wetu wote, kama tunampenda Yeye, hebu tuseme hivyo sasa.

Nampenda, (Ee Mungu!), Nampenda
Kwani . . .

63-1028 Msamaha
Ramada Inn
Tucson, Arizona Marekani

SWAHILI

©2020 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org